
SportPesa
TZS. 686,934,380
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SIMULIZI** ya mtoto miaka 3 kubakwa kisingizio cha soda





# Nipashe

Jumamosi Novemba 20, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580770

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


UKURASA 11

# Vita vya Samia vyazaa matunda



**NI** kuhusu wanaoharibu vyanzo vya maji, raia wa China anaswa akivuta lita milioni moja, saa nne kumwagilia mboga...*Endelea ukurasa wa 2*





Ofisa wa Maji Msaidizi Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, Halima Faraji (kushoto), akiangalia mashine ya kuvuta maji Mto Ruvu, waliyoikamata ikitumiwa na mkulima wa mboga raia wa China, Guoxian Gwen, katika Kijiji cha Kidogozelo, Chalinze, mkoani Pwani jana, ikitumika kumwagilia katika shamba lake lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 50. Kulia ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Kidogozelo, Salum Mambeche. **Picha kulia:** Mkulima Guoxian Gwen akiwa chini ya askari polisi baada ya kukamatwa. **PICHA: FRANK MONYO**

## CCM yaiagiza TAKUKURU kuichunguza Wizara ya Maji

UKURASA 3

## Wasira awataka vijana kuhoji mambo, kunyamaza ni unafiki

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA, NAMUNGO MUDA WA HUKUMU UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Vita vya Samia vyazaa matunda

Na Frank Monyo

SIKU MOJA baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuwatangazia vita wanaoharibu vyanzo vya maji, mkulima mkubwa raia wa China amenaswa akidaiwa kuchukua maji kutoka Mto Ruvu kwa kutumia mashine yenye uwezo wa kuvuta lita milioni moja.

Raia huyo wa kigeni anayefanya kilimo cha umwagiliaji, amekamatwa na Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu katika Kijiji cha Kidogozelo, Chalinze mkoani Pwani.

Ofisa wa Maji Msaidizi wa Bonde hilo, Halima Faraji, alisema jana kuwa mtu huyo alikamatwa katika doria waliyoifanya Novemba 12, mwaka huu baada ya kumbaini mkulima huyo wa mboga kutumia maji ya Mto Ruvu bila kibali. Baada ya kumkamata alitozwa faini ya Sh. milioni tatu.

"Cha kwanza tulimkagua na kubaini hana kibali cha Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu kutumia maji ya mto. Tulichukua mashine yake na tukamtaka afike ofisini kwa ajili ya kulipa faini. Novemba 15, akifika ofisini na kulipa faini na tukamzuia kuendelea na umwagiliaji.

"Leo (jana) tena tumefika eneo hili tumekuta kafunga mashine nyingine mpya anaendelea kuvuta maji mtoni," alisema.

Faraji aliongeza kuwa mkulima huyo aliwahi kuomba kibali cha kutumia maji miaka mitano iliyopita lakini hakuwahi kufuatilia na badala yake akawa anaendelea na kilimo cha umwagiliaji katika eneo hilo kinyume cha sheria.

Alisema anachofanya mkulima huyo ni uharibifu mkubwa kwa kuwa anatumia zaidi ya saa nane kuvuta maji kutoka Mto Ruvu kumwagilia, wakati kwa sasa kuna upungufu mkubwa wa maji katika mto huo unaosababisha mgawo wa maji katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

"Anachokifanya kina athari kubwa. Moja, hii mashine ameifunga karibu na mto kabisa na kitendo hiki kinachafua maji ya mto kwani mafuta ya dizeli katika mashine yanaingia ndani ya mto na kusababisha uharibifu mkubwa na uchafuzi wa maji. Athari nyingine anatumia maji mengi sana kwani anamwagilia saa nane kwa siku," alisema,

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Bonde hilo, Hhau Sarwatt, alisema baada ya doria za mara kwa mara maji yameongezeka kwenye mto huo.

Alisema kwenye doria hizo, walikuwa wakiendelea kutoa elimu kwa wafugaji na wakulima hili wasiharibu kingo za mto Kwa kuingiza mifugo kwenye mito.

"Baada ya kufanya doria katika mito mara kwa mara na kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji juu ya matumizi sahihi ya maji, tumeona maji yameanza kuongezeka Mto Ruvu. Lakini sasa huyo mkulima anachokifanya hapa ni uharibifu mkubwa kwani anachukua maji mengi sana kwa saa wakati kwa sasa kuna shida ya maji," alisema.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akikagua gwaride la Kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia, kabla ya kukizindua rasmi kikosi hicho, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Wasira ataka vijana kuhoji, asema kunyamaza ni unafiki

Na Romana Mallya

MWANASIASA mkongwe nchini na waziri aliyehudumu katika serikali tatu, Stephen Wasira, amewataka vijana kujifunza kuhoji na wasifikiri kunyamaza na kufanya unafiki ndio uzalendo.

Wasira aliyasema hayo jana Dar es Salaam, wakati wa kongamano la maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika liloandaliwa na Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere (MNMA), Kampasi ya Kigamboni.

Akizungumza katika mada isemayo "Uongozi na Maadili Katika Miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika", Wasira ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi wa Chuo hicho, aliwataka vijana wajifunze na wawe tayari kuhoji mahali ambako kunatakiwa.

"Msibaki mmenyamaza tu na mkafikiri kunyamaza na kufanya unafiki kuwa ndio uzalendo. Uzalendo wa namna hiyo hauna maana, tena siutaki kabisa. Uzalendo wa unafiki? Hapana, ndiyo maana wengine tumekuwa tunahoji.

"Nimefanya kazi na Mwalimu Julius Nyerere (Baba wa Taifa) na watu wengine walifikiri Mwalimu hawezi kuulizwa, lakini si kweli. Kuna siku nilimwuliza,"alisema.

Pia aliwataka vijana waendelee kujifunza maadili na historia ya nchi hata kama ni kwenye mitandao wasome na kuchuja.

"Tumewajengea nchi tunaweza tukawa hatujafikia lengo lakini tumejenga chini ya uongozi Mwalimu Nyerere. Kuijenga nchi yenye umoja, kubwa mnaweza kutukosoa unayotafakari kwa miaka 60 lakini bado tutakwambia tumejenga nchi," alisema.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema majukumu ya chuo hicho ni pamoja na kufundisha fani mbalimbali za kitaaluma na kutoa mafunzo ya uongozi, maadili, uzalendo na utaifa.

Alisema jukumu lingine ni kutoa elimu ya kujiendeleza, kufanya utafiti ambao unatoa majibu ya matatizo yanayoikabili jamii, kutoa ushauri wa kitaalam kwa sekta binafsi na serikali kwa kutoa wataalam.

"Mchango wa wanawake hasa katika historia ya nchi hii ni jukumu la chuo kupitia watafiti kuhakikisha wanafanya utafiti wa wale wote ambao wamechangia kwa kiwango kikubwa katika uhuru wa nchi hii," alisema.

Prof. Mwakalila alisema kwa kupitia utafiti huo, kunakuwa na machapisho ambayo yatasomwa na watu mbalimbali ili kila mtu ambaye hajui mchango wa wanawake, atafahamu.

"Mwakani Chuo kinategemea kuwa na kongamano la kitaaluma la kitaifa na kimataifa ambalo litakuwa na mada mbalimbali za kitaaluma.

"Ninatoe wito kwa wahadhiri wa chuo hiki, akiwamo Mkuu wa Idara ya Jinsia (Dk. Sarah Mwakyambiki), aliyetoa hoja ya kuwatambua wanawake katika historia ya nchi. Niwaombe wahadhiri walifanyie kazi jambo hili," alisema.

## Matumizi dawa za kulevya yaongezeka

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ( DCEA), imesema tatizo la matumizi ya dawa za kulevya nchini bado kubwa na kwamba kwa sasa watumiaji wa dawa ya kulevya aina ya heroine wanakadiriwa kufika 500,000.

Kutokana na ongezeko hilo, imewaomba Watanzania kuwafichua watu wanaojihusisha na biashara ya uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya ili DCEA iwakamate na kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi vifaa kwa ajili ya uendeshaji wa kliniki ndogo ya kutoa huduma kwa waraibu wa dawa za kulevya kwa wafungwa, mahabusu katika Gereza la Segerea.

"Watanzania msaidiane na DCEA katika kutoa taarifa nani anatumia nani anafanya biashara hii. Katika haya mapambano hatuogopi mtu, hata kama ni mapapa sisi hatutachoka kufanya kazi, nyie tupeni taarifa kisha muone tutakachofanya," alisema Kusaya.

Kamishna Kusaya alisema katika mkoa wa Dar es Salaam kuna kliniki nne zilizoanzishwa kwa ajili ya kutoa huduma ya uraibu kwa watuamiaji wa dawa za kulevya. Alisema kwa nchi nzima kuna vituo 11.

Alisema idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya wanaopewa huduma ya matibabu katika vituo hivyo wamefikia 10,600, hivyo kusababisha baadhi ya vituo kuzidiwa kutoa huduma.

Alisema lengo la DCEA ni kuhakikisha kila mkoa unakuwa na kliniki ya kutoa matibabu, hivyo kituo hicho kipya kitawawezesha mahabusu, wafungwa na wananchi wanaoishi jirani na Gereza la Segerea kuja kupata huduma hiyo.

Kusaya alitaja vifaa walivyokabidhi katika kituo hicho ni kabati la chuma la kuhifadhia dawa, photocopy mashine, printer, computer, makabati ya kuhifadhia mafaili, kitanda cha kumpimia mgonjwa, plastiki za kutandikia kitanda.

Vingine ni vipimo vya kupimia pombe, mabomba ya sindano, vikombe vya kunywa dawa, meza, viti, vipimo vya kupimia mkojo, kipimo cha kupimia shinikizo la damu.

Naye Daktari Mfawidhi wa Hospitali Kuu ya Magereza, ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa Methadone, Dk. Abdilatifu Mkingule, alisema: "Tulikuwa na mkakati wa kuanzisha kituo hiki miaka mitano iliyopita, mchakato ulikuwa mrefu, tumepitia changamoto nyingi."

Alisema walikuwa wanapata changamoto nyingi katika kuwahudumia wafungwa ambao ni watumiaji wa dawa za kulenya, hivyo kuanzishwa kwa kituo hicho kutatua changamoto hiyo.

Alisema: "Tuna zaidi ya magereza 10 yanayohitaji huduma kama hii, tunatamani huduma hii ifike katika magereza yote nchini kwa sababu idadi ya wanaohitaji ni wengi."

# HABARI KITAIFA

## CCM yashtuka wananchi kuingia wodini bila viatu

**Na Beatrice Shayo,** KIGOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Christine Mndeme, ameagiza ufanyike uchunguzi dhidi ya watumishi wa afya wilayani Uvinza mkoani Kigoma wanaodaiwa kuwataka wananchi kuvua viatu wanapoingia wodini kusalimia wagonjwa wao.

Mndeme alitoa agizo hilo juzi alipozungumza na wananchi katika shina namba moja na Tawi la CCM Nyakatakala A wilayani humo.

Alisema mtumishi atakayebainika kutoa agizo hilo kinyume cha utaratibu, hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.

"Hii ni kero ambayo kinamama inawasumbua kuwaambia kuvua viatu wanapoingia wodini, wanachohofia inawezekana wakaondoka na magonjwa," alisema Mndeme.

Alimwagiza mkuu wa wilaya hiyo kuanza kuchunguza jambo hilo la wanawake kulazimishwa kuvua viatu wanapoingia wodini, kitendo ambacho alisema ni kinyume cha taratibu.

"Uchunguzi ufanyike kubaini nani aliyetoa maagizo hayo na kwa sababu zipi na hatua kali za kinidhamu zichukuliwe kwa mhusika aliyetoa maagizo hayo ya kuvua viatu.

"Ni mtu mmoja ameamua watu wasiingie na viatu. Hospitali gani watu huwa tunaingia bila kuvaa viatu? Hakuna hospitali ambayo watu wakienda wanavua viatu," alisema.

Mndeme alisema suala hilo limeleta ukakasi na ni vyema hatua zikachukuliwa ili kulinda afya za wananchi hao pindi wanavyowatembelea wagonjwa wao.



Mtumishi wa Hospital ya Taifa Muhimbili (MNH), Robert Lukanga, akiwa juu ya pikipiki yake aina ya Hunter, aliyoshinda kwenye promosheni ya Kopa na Ushinde inayoendeshwa na Taasisi ya Kifedha ya Bayport Financial, baada ya kukabidhiwa jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Meneja Masoko na Mawasiliano wa Bayport, Ngula Cheyo na Mwakilishi wa Ofisa Utumishi wa MNH, Abdallah Kiwanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simulizi mtoto miaka mitatu kubakwa kisingizio cha soda

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MTOTO mwenye umri wa miaka mitatu, mkazi wa mtaa wa Mji Mwema, mjini hapa, amefanyiwa kitendo cha ubakaji na mtu asiyejulikana kwenye vichaka jirani na stendi mpya ya mabasi.

Akizungumza na Nipashe jana, nyumbani kwa mwathirika, kaka yake, mwenye umri wa miaka mitano, alisema wakati akiwa anacheza na mdogo wake na mtoto mwengine, alitokea mwanamume aliyekua amebeba begi mgongoni na kuwaambia wamwache (mwathirika) halafu wao wakaangalie kama soda zinapatikana maeneo hayo.

"Wakati tunacheza, alikuja baba mmoja, mimi simjui, akasema nendeni mkaangalie soda kama zipo mje mchukue hela mkanunue. Mimi na mwenzangu tukakimbia kwenda lakini tulivyorudi tukakuta mdogo wangu hayupo," alisema mtoto huyo.

Mtoto huyo alisema walimtafuta mdogo wake pasipo mafanikio, hivyo alisubiri mama yao arudi ili amwambie. Naye mama wa mtoto huyo, Imani Msambwa, alisema aliondoka nyumbani Novemba 11, mwaka huu, majira ya saa 2:00 asubuhi kwenda shambani akiwa amewaandalia chakula.

"Nilivyoenda chambani nikirudi majira ya saa 11:00 jioni, jirani mmoja akaniuliza mtoto yuko wapi uneenda naye shambani mbona kaka yake alikuwa anamtafuta? Mimi nikasema sijaenda naye nilimwacha ndipo nikaanza kumtafuta pasipo mafanikio. Mpaka saa 1:00 jioni nikaenda kwa balozi kutoa taarifa," alisema mama wa mtoto huyo.

"Nilimtumia baba yake message nikamwambia mtoto simwoni yeye alikuwa shambani Kidete ni mbali na hapa, akasema tutafute tukikosa twende kituoni asubuhi. Tuliendelea kumtafuta hadi saa tatu usiku tukafika nyumba moja jirani na stendi mpya yule mama akasema kuna mtoto ameokotwa akitokea porini amefanyiwa kitendo kibaya na amepelekwa hospitali ya Kibena. Nikajiandaa nikaenda nikakuta mtoto ndiye yeye," alisema Imani.

"Kujua amefanya nani hili tukio ni ngumu kwa sababu wakati anachukuliwa alikuwa na wenzake wawili na ukimuuliza kaka yake anasema alikuja baba amebeba begi na mtoto ukimuuliza anakwambia alikuwa baba amebeba begi," alisema Imani.

Naye bibi wa mwathirika, Jane Kichungula, alisema wanaoishi vizuri na majirani hakuna ugomvi, hivyo wanashindwa kujua kwa nini jambo hilo baya limeikumba familia yao.

Naye Balozi wa Msete, Mtaa wa Mji Mwema, Agustino Mfikwa, alisema hilo ni tukio la kwanza katika eneo lake na kwamba zamani simba ndio alikuwa akiogopwa lakini hivi sasa binadamu anatisha zaidi.

"Ukiondoka kidogo tu huku nyumba umevamiwa. Tunaiomba serikali kuelimisha maana sisi wanadamu tumekuwa tofauti sana. Kumwingilia mtoto mdogo kama huyu nini unafaidi? Ni ujambazi tu," alisema Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema ni kweli tukio hilo limetokea na mama wa mtoto huyo alikwenda shambani asubuhi na kumwacha mwathirika na kaka yake ili amwangalie.

"Mama aliporudi nyumbani hakumkuta mtoto ila baada ya kutafuta alitokea msamaria mwema alimwokota mtoto akitokea vichakani huko nyuma ya stendi mpya huku analia na tayari alikuwa ameingiliwa na mtu ambaye hajulikani. Matokeo yake mtoto huyu amebakwa na kulawitiwa, kwa hiyo mpaka sasa mtoto tunaye hospitalini anaendelea na matibabu," alisema.

Kamanda Issah alisema Jeshi la Polisi bado linaendelea na uchunguzi ili kumbaini mtu ambaye amemfanyia kitendo cha ukatili mtoto huyo.

Hata hivyo, alitoa rai kwa wananchi kwamba pamoja na shughuli za kiuchumi, wahakikishe ulinzi kwa mtoto hasa kipindi hiki cha kilimo.

## TAKUKURU yaagizwa kuichunguza Wizara ya Maji

**Na Beatrice Shayo,** KIGOMA

CHAMA Cha Mapindunzi (CCM) kimeiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi katika Wizara ya Maji kutokana na makandarasi kutimka na kuacha kuendelea na ujenzi wa miradi nchini.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Shaka Hamidu Shaka, alitoa maagizo hayo jana mkoani Kigoma alipotembelea mradi wa kitekeo cha maji Ziwa Tanganyika.

Alibainisha kuwa katika maeneo aliyotembelea makandarasi wamejitoa na kusababisha miradi kukwama na wananchi kupata vikwazo katika kupata huduma hiyo. Shaka alisema kuna haja taasisi hiyo kufanya uchunguzi kwa kitendo cha makandarasi kujitoa katika miradi ya maji nchini ili kuepuka miradi kuchelewa kukamilika.

Alisema katika mradi huo wa maji wa Ziwa Tanganyika mkandarasi mmoja alijitoa kufanya kazi huku wakiwa tayari wamefanya upembuzi yakinifu na kukubali kufanya kazi.

"Hapa sasa ni mtu mmoja kashajitoa na huyu aliyepo ni wa pili. Hii ni shida kubwa ya makandarasi kuondoka. Niliongea na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliniambia anakusudia kukutana na makandarasi nchi nzima, ninadhani hili nalo muhimu," alisema.

Shaka alisema serikali inawapa kazi makandarasi wa nchini kwa kuwaamini, lakini wanairudisha nyuma kwa kitendo cha kujitoa kwenye miradi. Alisema kwa sasa jicho la chama hicho litakuwa katika mradi wa maji wa Ziwa Tanganyika kuona namna gani utekelezaji wa ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan unafanyika kuhakikisha wananchi wanapata maji.

Shaka alisema njia pekee ya kukabiliana na tatizo la maji katika mikoa iliyopo karibu na ziwa ni kuhakikisha serikali inakamilisha miradi mikubwa iliyojiwekea.

Alisema ni jukumu la msingi kwa Wizara ya Maji hususani kwa ofisi zilizopo kwenye mikoa yenye ziwa kuhakikisha wanapunguza au kutatuashida ya upatikanaji wa maji kwa wananchi.

"Wizara ya Maji, hili ni jukumu lenu la msingi hasa nyie mliopo ziwani, tunataka tutoka huku sasa sababu kimbilio pekee la kupunguza au kutatua changamoto ya maji ni kutumia rasilimali hii ya ziwa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Maji Kigoma (KUWASA), Mbike Jones, alisema mradi huo unasimamiwa na Wizara ya Maji na mkandarasi wa kwanza, Spencon Service Ltd, aijitoa kuendelea na ujenzi wa kitekeo kipya cha maji katika eneo la Amani Beach.

Alisema mkandarasi wa pili, Sino-Hydro Corporation Ltd, alitia saini mkataba Novemba 23 mwaka jana na kuanza kazi Julai 19 mwaka huu na mradi umefadhiliwa na Umoja wa Ulaya na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW).


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA(MARUDIO)

***Kwa Idhini tuliyopewa na BANK OF AFRICA*** Tunatoa notisi ya siku saba (7) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | BEATUS ASSEY | ALBINA TESHA | Nyumba ya makazi yenye Hati ya usajili na.86073 Kiwanja na.5 kitalu"S" iliyopo Goba Tegeta | 30/11/2021 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:** **AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) Ltd**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor**
**P.O. BOX 1088**
**Dar Es Salaam.**
**Mob: + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Bank of Africa**
**Head Office,**
**NDC Development House, Ohio street/kivukoni**
**P.O. BOX 3054,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255-22-2110104/2111290**
**Fax: +255-22-2113740**

# Lumumba ahimiza uwazi matumizi fedha za corona

**Na Sanula Athanas,** ARUSHA

MWANAZUONI mashuhuri wa Kenya, Prof. Patrick Lumumba, amezishauri nchi za Afrika kuhakikisha kunakuwa na uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha wakati huu wa mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Prof. Lumumba alitoa rai hiyo jana jijini Arusha wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji, alipowasilisha mada kuhusu kuwapo ama kutokuwapo kwa uwazi na uwajibikaji kwa nchi za Afrika wakati wa janga hilo.

Mkutano huo wa siku mbili ulioanza juzi, uliandaliwa na Taasisi ya WAJIBU inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Ludovick Utouh, aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

"Sidhani kama kuna nchi yoyote barani Afrika imefanya tathmini ya matumizi ya fedha wakati wa mlipuko wa virusi vya corona. Mtakumbuka kilichotokea kwenye Bunge la Nigeria wabunge walipohoji matumizi ya fedha," alisema.

Prof. Lumumba alisema bila kuwapo uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha kipindi hiki cha corona, kuna hatari nchi nyingi za Afrika kukumbwa na matumizi mabaya ya fedha miongoni mwa viongozi wake.

Alionya kuwa kama hakutakuwa na uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha kwa kisingizio cha kupambana na corona, nchi nyingi barani Afrika zitakumbwa na dosari ya kiusalama, akifafanua kuwa vijana wengi watakosa ajira, hivyo kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu.

Mwanazuoni huyo pia alisifu uamuzi wa Tanzania kuachana na utaratibu uliokuwa unatumiwa na nchi nyingi wa kutangaza takwimu za wagonjwa wapya na vifo vitokanavyo na corona, akisisitiza kuwa ndiyo umeisaidia nchi kutoyumba kwa kiwango kikubwa kiuchumi.

"Corona imetuonyesha udhaifu tulionao kwenye sekta ya afya. Kule kwetu Kenya tumebaini kumbe tuna mitungi michache sana ya oksijeni na ICU (wodi za wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalam) ni chache.

"Mikutano mingi ya mawaziri kujadili corona haikuwa na maana. Mawaziri wetu katika nchi za Afrika waliishia kusoma takwimu na kututangazia 'leo tuna wagonjwa wapya wengi'. Hii ilitengeneza hofu kubwa.

Ninaipongeza Tanzania kwa hatua ilizochukua kuachana na utaratibu huo. Ulikuwa uamuzi sahihi sana, Burundi pia ilifanya hivyo. Corona ipo na tutaishi nayo kwa muda mrefu. Mpaka leo Uganda ninaambiwa bado shule zimefungwa," alisema.

Prof. Lumumba pia alitoa angalizo kwa nchi za Afrika kujiandaa kuachana na utegemezi, akifafanua kuwa kwa sasa kuna kile alichokiita 'vita vya kutengenezwa' katika baadhi ya nchi zikiwamo Cameroon, Somalia na Ethiopia.

"Afrika ikiwa dhaifu ni furaha kwa China, Afrika ikiwa na vita ni furaha kwa Ulaya na Amerika. Sisi (Afrika) ni dhaifu na hatuna hata vifaa vya kujiridhisha kuhusu ubora wa vitu tunavyoletewa," alihitimisha.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya mipaka ya Tanzania, wakiwamo mawaziri, wabunge na viongozi wa taasisi za serikali na zisizo za kiserikali.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuza Ludigija (wa nne kulia), akipokea vifaa vya kufanyia usafi kutoka kwa Ofisa Mradi wa shirika la WaterAid Tanzania, Rebecca Stanley (wa nne kushoto), kwa ajili ya mitaa ya Buguruni na Hospitali ya Chanika-Nguvukazi, kwenye maadhimisho ya Siku ya Choo Duniani, yaliyofanyika Chanika wilayani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yajivunia mchango wa Ofisi ya Msajili wa Hazina

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itaendelea kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina bila kuchoka kwa kuwa ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Pia serikali imeipongeza ofisi hiyo kwa kazi nzuri ya usimamizi wa taasisi na mashirika ya umma, maeneo ambayo serikali imefanya uwekezaji mkubwa ili hatimaye ulete tija na kuendelea kutoa mchango wa ukuaji kiuchumi na kustawisha maendeleo ya nchi.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais -Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro, alisema hayo jana wakati akifungua Mkutano wa Kwanza wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mwaka 2021/22, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kukaribishwa na Mwenyekiti wa Mkutano huo, Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, Dk. Ndumbaro alisema; "Ni ukweli usiopingika kuwa kutokana na majukumu makubwa ya kusimamia takribani mashirika na taasisi za umma 237, kampuni 50 ambako serikali imewekeza mtaji wake kwa utaratibu wa hisa. Pamoja na kusimamia mashirika ya umma, viwanda na mashamba 341 yaliyobinafsishwa, Ofisi ya Msajili wa Hazina ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu."

Dk. Ndumbaro aliongeza kuwa watumishi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina wanapaswa kuzingatia kuwa nchi inawategemea katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, kupunguza matumizi na kuimarisha utawala bora kupitia usimamizi madhubuti wa mashirika na taasisi za umma, hivyo ili kufikia malengo hayo, wanapaswa kutimiza wajibu wao kikamilifu.

"Kila mtumishi katika Ofisi ya Msajili wa Hazina anapaswa kutambua wajibu wake kwa Taifa na kujitambua kuwa ana umuhimu katika kuwezesha taifa kufikia malengo yake.

"Endeleeni kufanya kazi kwa bidii, uadilifu, weledi na uzalendo mkubwa katika kusimamia rasilimali za umma mlizopewa dhamana ya kuzitunza na kusimamia ili zilete tija na kuongeza mapato yasiyo ya kodi kuchangia mfuko mkuu wa serikali kuwa na uwezo wa kuboresha huduma kwa wananchi na maslahi ya watumishi wote," alisema.

Awali, Msajili wa Hazina alimshukuru yeye binafsi kwa kukubali mwaliko na kushiriki kikao cha Baraza la Wafanyakazi lakini pia serikali kwa kuendelea kuiamini ofisi yake katika usimamizi wa mashirika na taasisi za umma.

Mgonya alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumteua kuwa Msajili wa Hazina ili kuendeleza jukumu la usimamizi wa rasilimali za nchi zinazotokana na uwekezaji wa serikali. Msajili wa Hazina, katika mkutano huo, aliwasilisha mambo mbalimbali ambayo ofisi imeyatekeleza katika kuimarisha usimamizi wa mashirika ya umma, lakini pia aliwasilisha mikakati iliyopo katika kuimarisha usimamizi kwenye Mashirika na Taasisi za Umma ili mchango wa uwekezaji wa serikali uweze kuleta tija kwa maendeleo ya nchi.

Alisema ufanisi wa usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina umejidhihirisha katika maeneo mengi, akitolea mfano ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kuwa katika kipindi cha miaka minne cha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21 mapato yameongezeka kutoka Sh. bilioni 161.03 hadi Sh. bilioni 637.67.

Kwa mujibu wa Mgonya, mapato haya ni yale tu yanayopitia akaunti za Ofisi ya Msajili wa Hazina na kwamba endapo yangejumuisha na yale yanayokwenda moja kwa moja kwenye mfuko mkuu wa serikali, yangepaa zaidi akitolea mfano kabla ya janga la corona mapato yalifikia Sh. trilioni 1.052 mwaka 2018/19.

## Ndalichako akemea urasimu Utoaji habari

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako,amekemea urasimu unaofanywa na baadhi ya wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara kwa kutokutoa habari kutangaza mambo yanayofanyika.

Kutokana na hali hiyo, amewaagiza wakuu wa taasisi hizo kuwapa mamlaka maofisa habari kufanya majukumu kwa kutoa habari ili kuelezea kazi kubwa inayofanywa na wizara katika sekta ya elimu.

Prof. Ndalichako alitoa agizo hilo, katika kikao kazi kilichowakutanisha wakuu wa taasisi, maofisa mawasiliano ya umma na maofisa habari wa taasisi mbalimbali za elimu nchini, kilichofanyika mjini hapa.

Alisema Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa wizara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu nchini lakini haisemewi katika vyombo vya habari kutokana na urasimu kutoka kwa wakuu wa taasisi ambao hawawapi nafasi maofisa habari wao kuelezea kwenye vyombo vya habari.

Alisema urasimu wanaofanyiwa maofisa habari na wakuu wa taasisi hizo haukubaliki na kuwataka wakuu hao kuwapa fursa maofisa mawasiliano kutumia nafasi zao ili kusemea miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali.

Aidha, aliwataka maofisa mawasilinao na maofisa habari kutangaza mafanikio ya sekta ya elimu ili wananchi wafahamu serikali ilivyowekeza fedha nyingi katika maendeleo ya elimu nchini.

Ndalichako alisema mafakinio katika sekta ya elimu ni makubwa na si ya kificho, hivyo ni vyema wananchi wakafahamu ni namna gani serikali ilivyowekeza katika kuhakikisha elimu bora inatolewa.

Prof. Ndalichako alisema mara nyingi amekuwa akishuudia maofisa mawasiliano wanajielekeza zaidi katika kutangaza matukio ya viongozi wanapokuwa katika shughuli mbalimbali kwenye taasisi zao na baada ya matukio hayo hakuna kinachoendelea.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, aliwataka maofisa habari na maofisa mawasilino ya umma, kutekeleza majukumu yao kwa kupanga mikakati ya utendaji kazi wa kisasa ikiwa ni pamoja na kutumia mitandao ya kijamii ili kuboresha taarifa kuwafikia wananchi kwa uharaka zaidi na kuacha kusubiri matukio ya viongozi.

Naye Mkuu wa Mawasiliano na Habari kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk Dotto Kuhenga, alisema kuna umuhimu wa wanahabari kufahamu kazi za taasisi zao ili kutoa taarifa kwa ufasaha zaidi na si kusubiri kuwapo kwa upotoshaji katika mitandao ya kijamii ndipo watoe ufafanuzi.

## TANGAZO



# Ndoto zinatimia na kuwa kweli Tanzania kupitia Dream Maker ya betPawa

Watanzania 13 wanaishi ndoto zao sasa hivi kwa msaada wa betPawa Dream Maker.

betPawa ilitembelea nchi ndani ya Dream bus, kuhamasisha watu kutushirikisha katika ndoto zao. Ndoto zote zilizo wasilishwa zilipitiwa kwa umakini na zile ambazo zinahamasisha zaidi zinatimizwa.

Basil anajengewa nyumba ya wazazi wake, ambayo iliharibika kutokana na mafuriko. ‘’Hii itakua ni ndoto ya maisha yangu. Hiki ni kitu muhimu sana kwangu,’’ Alieleza.

Kocha wa mpira wa kikapu Boaz anajenga uwanja wa kisasa wa kikapu ili kila mtu katika jamii aweze kucheza.

Alisema,’’Watu wa umri wowote, jinsia, hali ya kijamii au kiimani watakuja pamoja’’

Erick anafungua ukumbi wa kuangalia michezo moja kwa moja. Alieleza “Hii ni ndoto niliyokuwa nayo muda mrefu sana. Kupitia Dream maker, nitawafanya na ndoto za wengine pia kutimia.”

Kazi ya Dream maker haikuhisha hapo. Athumani, Chacha, Clement, Edwin, Juma, Lusungu, Paul, Rayah, Steven na Upendo nao ndoto zao zilifanikiwa kuchaguliwa pia.

Fuatilia safari ya wenye
Ndoto kupitia **betpawadreamers.com/tanzania**

**betPawa**

Cheza kiasi. 18+. betPawa imesajiliwa chini ya bodi ya michezo ya kubashiri ya Tanzania. Leseni #SBI000000026.

216579002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ligi Kuu Bara irejee na burudani si 'mauzauza'

**LIGI** Kuu ya NBC Tanzania Bara imerejea tena kuanzia jana kwa timu nne kushuka dimbani kupambana wakati leo Jumamosi mechi nyingine tatu zinatarajiwa kuchezwa kwenye viwanja tofauti hapa nchini.

Mbali na ligi hiyo, pia Ligi Kuu ya PBZ Zanzibar nayo imerejea kuanzia jana na kesho itaendelea kwenye viwanja mbalimbali vya Unguja na Pemba.

Ligi hizo zilisimama kupisha kalenda ya kimataifa ya Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), ambapo mataifa mbalimbali yalikuwa yanapambana kucheza mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali za mwakani za Kombe la Dunia huko Qatar.

Kwa upande wa Tanzania, Timu ya Taifa maarufu Taifa Stars yenyewe imeshatolewa kwenye kinyang'anyiro hicho baada ya kushindwa kuzichanga vyema karata zake.

Taifa Stars inayonolewa na Kim Poulsen, raia wa Denmark, ilimaliza mechi za hatua ya makundi ikiwa kwenye nafasi tatu ikiwa na pointi nane, nyuma ya vinara Jmahuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), waliofikisha pointi 11, Benin waliokuwa na pointi 10 na Madagascar iliburuza mkia ikiwa na pointi nne.

Mbali na timu za Afrika, pia Ulaya mataifa mbalimbali nao walikuwa kwenye mchakato huo na baadhi ya timu tayari zimeshakata tiketi ya kwenda Qatar huku nyingine sawa na mataifa 10 ya Afrika yakisubiri hatima yao baada ya kucheza michezo ya hatua ya mtoano ambayo itachezwa Machi mwakani.

Hayo yamemalizika, waliofanikiwa wamefanikiwa, na waliokosa tiketi ya kushiriki fainali hizo zinazokuja, bado wana nafasi ya kukaa na kutafakari pale walipokosea ili kuanza kujiimarisha kwa ajili ya mashindano mengine yatakayochezwa 2026.

Tunaamini mbali na Taifa Stars kushindwa kutimiza ndoto zake kama ilivyotarajiwa, lakini kuna baadhi ya mambo ambayo wachezaji, viongozi, wadau na mashabiki wa soka Tanzania wamejifunza kupitia michuano hiyo mikubwa iliyoko mbele yetu.

Nidhamu ambayo ilionekana kwa timu zote zilizokuwa zinashiriki michuano hiyo iwe fundisho kwa wachezaji wa hapa nchini ambao siku moja nao wanatakiwa kupata nafasi ya kupeperusha bendera ya taifa.

Hakuna timu ambayo inaweza kuvuna matokeo chanya kama haikuwa na maandalizi bora au wachezaji wenye viwango vya juu ambao wanaweza kushindana.

Umefika wakati kwa wachezaji wanaoshiriki katika ligi mbalimbali za hapa nchini wakajituma na kucheza kwa bidii ili kuonekana na mawakala wa nje na hatimaye kusajiliwa na timu zinazoshiriki ligi zilizoendelea.

Viwango na ufundi vilivyoonyeshwa na wachezaji wa Afrika wanaocheza kwenye Ligi za Ulaya vimesaidia kwa kiwango kikubwa kuzibeba timu zao, hivyo hilo ni somo kwa nyota wa hapa nchini kuendelea kujituma na kusajiliwa Ulaya na baadaye watakaporejea kuitumikia Stars, wanakuja wakiwa imara na walio tayari kwa mapambano.

Kama ambavyo tumeshuhudia vikao vya maandalizi ya mchezo, namna timu zilivyoingia uwanjani, tunatarajia hayo pia yaonekane kwenye mechi za Ligi Kuu ya NBC Tanzania, Ligi ya Championiship ambazo huzalisha idadi kubwa ya wachezaji wanaoitwa kwenye kikosi cha Stars.


Wachezaji wanatakiwa kuamini soka safi ndiyo huzalisha matokeo chanya na kamwe si kufanya vitendo vya kishirikina kama tutahitaji kufika kule ambapo Waafrika wenzetu kutoka Algeria, Tunisia au Nigeria walipo.

Tutumie kile tulichojifunza katika mechi za kimataifa kuzipa heshima ligi zetu kwa sababu msingi imara wa mchezaji huanzia sasa na si kusubiri ngazi ya juu ambayo ataifikia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Chendacho mavani hakina marejeo

Na Barnabas Maro

**MAVA** ni makaburi. Kinachoenda makaburini hakiwezi kurudi tena. Mathalani mtu aliyekwisha kuzikwa makaburini hawezi kuwa hai tena. Methali hii hutumiwa kutufunza kitu kinachotaliwa na anayetuzidi nguvu hatuwezi kukipata tena. Pia tunahimizwa tuvitunze vizuri vitu tulivyonavyo.

Aidha, "Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine. Tunafunzwa tuvitegemee vitu vyetu na wala si vya watu wengine . Tunasihiwa tuvithamini vitu vyetu ingawa sio vizuri kama vya watu wengine.

Vile vile tunaambiwa "Chako kikioza hakinuki (unakianikaanika). Maana yake kitu chako kikisha haribika unajaribu kukishalikishaliki (rekebisha ili kifanye kazi vyema.)

Neno "fedha" lina maana tatu; 1. Madini yenye rangi ya kijivu - nyeupe. 2. Metali ya thamani inayotumiwa kutengenezea sarafu, vito au vitu vya mapambo. 3. Sarafu ambayo hutumika kulipia huduma;=pesa, hela.

Ndio maana wahenga walisema "fedha ilivunja nguu, milima ikalala." Kwamba fedha zina uwezo wa kuvunja milima na vilima.

Methali hii hutumiwa kupigia mfano uwezo wa fedha. Mtu akiwa na fedha anaweza kufanikiwa kufanya mambo ambayo asingeweza kuyafanya wala kudhania kuyafanya.

Nina sababu ya sababu ya kutumia methali mbalimbali kuhusu uwezo wa fedha. Naam, penye nia pana njia." Ikiwa mtu ana dhamira ya kufanya jambo fulani hawezi kukosa njia.

Methali hii hutumiwa kutukumbusha tuwapo na nia ya kufanya jambo fulani, lazima tutafanikiwa. Wewe unayesoma makala hii waweza kukisia (kitendo cha kubahatisha dhati ya jambo;= dhania) ninachotaka kueleza?

**Methali hii hutumiwa kutukumbusha tuwapo na nia ya kufanya jambo fulani, lazima tutafanikiwa. Wewe unayesoma makala hii waweza kukisia (kitendo cha kubahatisha dhati ya jambo;= dhania) ninachotaka kueleza?**

Hapa nazungumzia vilabu vyetu vya kandanda nchini hasa Simba na Yanga, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Serikali tusidanganyane. Mpaka unaposoma makala hii, Tanzania imepoteza fedha nyingi ili kulipa mishahara mikubwa kwa wachezaji na makocha wa mchezo huo kutoka nje ya nchi ambao hulipwa maradufu ya fedha wanazolipwa wachezaji na walimu wa kandanda kutoka ughaibuni (mbali, nje ya nchi.)

Kwanini twapoteza fedha za nchi yetu masikini na kuwanufaisha watu wa nchi nyingine ilhali hali yetu ni dhaifu, yenye kutokuwa na nguvu na dhalili, yaani hali ya chini? Je, ni kweli kuwa Tanzania nzima hakuna wachezaji wanaoweza kusajiliwa na timu zetu hata tuwategemee wachezaji wa ughaibuni?

Wahenga walisema: " Ungapigia teo mtama waliwa." Maana yake mtama unaendelea kuliwa ijapokuwa unaendelea kuwapiga teo (munda) ndege.

Methali hii hutumiwa kupigia mfano wa mtu anayechelea kulifanya jambo vizuri inavyotakiwa au anayechelewa kuliwahi wakati unaostahiki. Huweza kutumiwa pale ambapo juhudi fulani hazielekei kuzaa matunda.

Tanzania kuna wachezaji wazuri sana ila tunashindwa kuwagundua kutokana na ubozi (upumbavu) wetu wa kudharau watu na vitu vyetu wenyewe. Matokeo yake kuna wachezaji kadhaa wazalendo wanaocheza kandanda nchi zingine kwa mafanikio makubwa.

Yasemwa "Tamaa mbele mauti nyuma." Maana yake ukiweka tamaa mbele mauti yatakuwa nyuma yakikufuata, mabaya yatakufuata. Methali hii hutumiwa kwa mtu mwenye tamaa nyingi. Wanadamu tunafunzwa madhara yanayoweza kutupata kutokana na tamaa isiyokuwa na mipaka.

Vilabu vyetu vya kandanda, TFF na Serikali wafanye tafakuri (mawazo mazito), kuhusu jambo hili kwani kuna wachezaji wengi walio tayari kuwa wanafunzi wa kandanda. Kazi kwenu.

**marobarnabas@yahoo.com**

# MATANGAZO

## NOTISI / TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBAGALA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | NYUMBA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | MBAGALA MWANAMTOTI | 14/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | ELIA MACHAKA ULEMA | NYUMBA | ELIA MACHAKA ULEMA | UNGINDONI KIGAMBONI | 15/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | GRACE ANTONY MGATA | NYUMBA | GRACE ANTONY MGATA | YANGE YANGE MSONGOLA | 16/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | SAMSONI MUSSA SAMANYI | NYUMBA | ZAKARIA WAMBURA NYAULE | MTAA MAJOHE VIWEGE | 24/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | FRANK SNART MWASHI | NYUMBA | FRANK SNART MWASHI | MTAA WA MAJOHE RADA | 22/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | MGINA HUSSEIN THABIT | NYUMBA | MGINA HUSSEIN THABIT | DODOMA | 07/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | JACQUILINE GAMARIELI JOHN | KIWANJA | JACQUILINE GAMARIELI JOHN | NZUGUNI | 08/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA (2) | DAVID ABEL MLAU&SADIKI NTAHONDI MAPORO | CHARAMBE & MKURANGA | 15/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | HASSAN SADIKI HILALI | NYUMBA | HASSAN SADIKI HILALI | TOANGOMA | 17/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | SEIF HAMAD NASSORO | NYUMBA | SEIF HAMAD NASSORO | MBAGALA | 15/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | AISHA HAMADI KIVINA | NYUMBA | AISHA HAMADI KIVINA | KIVULE MAJOHE | 21/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SAIDI AKILIMALI KALILWA | NYUMBA | SAIDI AKILIMALI KALILWA | MWASONGA KIGAMBONI | 08/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MWANAHAMISI KONDO MATAMBO | NYUMBA | MWANAHAMISI KONDO MATAMBO | RUVU DARAJANI | 10/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | AUGUSTINO KILUNDE SANGA | NYUMBA | AUGUSTINO KILUNDE SANGA | TANDALE | 14/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | GRACE ELIAS MAHUGI | NYUMBA | EMMANUEL KASANZU & GRACE MAHUGI | MBEZI MSIGANI | 15/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MARIAM PATRICK SHAYO | NYUMBA | DORICE YOHANA MWAKAPESA | MBEZI MSAKUZI | 16/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KINONDONI | ALLIANCE DISTRIBUTORS | NYUMBA | KANI ISAAC MRUMA | MALAMBA MAWILI | 21/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | REAL TASTE BAKERY | NYUMBA | THEODORY THEONEST BYABATO | KIBAMBA-UBUNGO | 07/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | MANENO MUSSA ISMAILI | NYUMBA | MANENO MUSSA ISMAILI | TEMEKE | 08/12/2021 KUNZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la Mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu **no.0784252048/ 0768672367/ 0754497396/ 0765999000/ 0715363537/ 0674821287**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

116580102

WaterAid

## TENDER No. PREQUALIFICATION/ PR/ 01/2021/2022 /2023

### Pre- qualification of Contractors for the Construction of WASH infrastructures in Kisarawe District

WaterAid is an International Non-Governmental Organization, with a vision of ensuring Safe Water Sanitation and Hygiene (WASH) for Everyone, Everywhere by 2030. WaterAid has had its operations in Tanzania since 1983 under the name "WaterAid Tanzania" which is registered as Non-Governmental Organisation in The Republic of Tanzania (NO.SO.7557).

WaterAid Tanzania (WAT) operates as a Country Programme and functional office of WaterAid UK; within East African Region. The head office is in Dar es Salaam, Rufiji Street, Plot No.1469, Masaki Area within Kinondoni District.

Water Aid Tanzania has received fund from the Japan International Cooperation Agency (JICA) for implementing a programme for Improvement of Hygiene Behaviour in Schools and Health Care Facilities. This project aims at improving access to WASH services and good hygiene behaviours in 30 primary schools and 15 health care facilities(dispensaries) in Kisarawe district.

Water Aid Tanzania invites applications from interested contractors who are registered by Contractors Registration Board (CRB) with class six, five and four for prequalification for the assignment of improving WASH infrastructures in Kisarawe District in Coastal Region from December 2021 to February 2022. The main works includes:

| Item | Activity Description | QTY |
|---|---|---|
| 1 | Construction/rehabilitation of sanitation facilities | 45 sites |
| 2 | Construction /rehabilitation of water supply systems/ schemes/ water points | 45 sites |
| 3 | Construction / rehabilitation of handwashing facilities | 45 sites |

Following documents should be submitted:

- Company profile that includes legal documents (Valid licenses and legal documentation to operate in Tanzania e.g. incorporation certificate, business license and relevant tax certificates, licenses from CRB.
- List of major equipment(s) for carrying out the works.
- A list of recent performed contracts of similar nature including the names and addresses of the employers for verification.
- Recent financial statements of the bidder/bank statement
- A duly Certified Power of Attorney

Eligible interested bidders should send their bids to WaterAid Tanzania Office before **24th November 2021** by 10:00am East African Time; through **ZuenaMasumay@wateraid.org**, Cc **NicombolweKidagho@wateraid.org**. Bids shall be addressed to: "Country Director – WaterAid Tanzania, P.O. Box 33759 Plot No.1469 Rufiji Street: Off Haile Selassie Rd - Msasani Peninsular, Dar es Salaam: Tanzania." and clearly marked **"Bid for Pre-qualification of contractors for the Construction of WASH infrastructures in Kisarawe District". The bids Opening will be on 24th November 2021 from 11:00am at WaterAid Country Office.**

***Note:*** *WaterAid has a Mandatory Operating Procedure (MOP) and therefore for those who will visit our office for, submision or tender opening will not be allowed to enter office premises without properly wash their hand and wearing masks*

116580302

# Wadaiwa kukiuka uuzaji wa madini

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA wa Dhahabu katika soko la madini hayo mjini hapa, wamelalamikia kitendo cha baadhi yao kununua bidhaa hiyo nje ya soko jambo ambalo ni ukiukaji wa utaratibu uliowekwa na serikali.

Pia wafanyabiashara hao wamesema kitendo hicho kinawaumiza wenzao ambao wametii agizo la kuuzia madini ndani ya soko hilo.

Malalamiko hayo yalitolewa jana na mmoja wa wafanyabiashara hao, Renatus Maji, aliyezungumza kwa niaba ya wenzake mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema hatua hiyo inawaumiza waliotii agizo la serikali la kufanyia biashara ya madini kupitia soko.

Maji alisema hali hiyo inawatia hasara kwa kuwa wote wamewekeza mitaji mikubwa kwa wachimbaji.

Kutokana na hali hiyo, alitumia mwanya wa mkutano wa mkuu wa wilaya na wafanyabiashara kuiomba serikali kudhibiti hali hiyo ili wateja wote wapeleke dhahabu katika soko hilo ili wote wafanye biashara yenye tija na kwamba serikali haitapoteza mapato yake.

Akijibu malalamiko hayo, Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Kahama, Jeremiah hango, alisema ofisa huyo alisema kuanzia sasa ofisi yake itafanya msako mkali kuwabaini wafanyabiashara wanaonunua dhahabu nje ya soko hilo ambao ni kinyume cha utaratibu uliowekwa na serikali badala yake aliwataka wajisalimishe na kuachana na tabia hiyo.

Hata hivyo, ofisa madini huyo katika mkutano huo uliofanyika eneo la soko la Madini, alimweleza mkuu wa wilaya kuwa ofisi yake imekusanya Sh. bilioni 34.88 sawa na asilimia 110 ya lengo la miezi minne kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema katika kipindi hicho, walipangiwa kukusanya Sh. bilioni 31 lakini kwa ushirikiano na wachimbaji, wamevuka lengo la serikali na kukusanya Sh. bilioni 34.88.

Kiswaga kwa upande wake alipongeza Ofisi ya Madini Kahama kwa kuvuka lengo la serikali walilopangiwa.

"RMO (Ofisa Madini Mkazi) na timu yako endeleeni kuchapa kazi kwani mmevuka lengo. Bajeti ilikuwa kukusanya Sh. Bilioni 31 lakini mmekusanya Sh. bilioni 34.88 na ninyi wafanyabiashara wa madini endeleeni kuchapa kazi kwa amani," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema yeye pamoja na kamati ya ulinzi na usalama atahakikisha wafanyabiashara hao wanafanya shughuli za madini kwa amani na utulivu huku akikaribisha wawekezaji wengine kuwekeza kwenye sekta ya madini katika wilaya yake.

# PAC yataka kasi usambazaji gesi majumbani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imetoa wito kwa serikali kuhakikisha kuwa suala la usambazaji gesi majumbani kuwa la kipaumbele.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya ziara ya kamati kutembelea miundombinu mbalimbali ya gesi iliyoko mkoani Mtwara, Pwani na Dar es Salaam.

Alisema usambazaji wa gesi hiyo majumbani, uzingatie kupeleka nishati hiyo kwenye maeneo yenye watu wengi ili kupunguza matumizi makubwa ya mkaa ambayo yanasababisha ukataji wa miti, hivyo kuchochea uharibifu wa mazingira.

Kuhusu ziara ya kamati hiyo kwenye miundombinu ya gesi, alisema kuwa kamati imeona uwekezaji mkubwa uliofanyika na kufurahishwa na wafanyakazi Watanzania wanavyoendesha na kusimamia miundombinu hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dk. James Mataragio, aliieleza Kamati hiyo kuwa kazi ya usambazaji gesi majumbani inaendelea katika mikoa mbalimbali.

Hata hivyo, alisema ili gesi hiyo isambazwe kwa wananchi wengi zaidi, wameanza kukaribisha kampuni binafsi ili kufanya kazi hiyo.

Ziara ya PAC ilikuwa na malengo mbalimbali ikiwamo kuona kama ujenzi wa miundombinu ya gesi iliyopo inalingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Wajumbe wa PAC walitembelea mitambo ya kuchakata gesi ya Mnazi Bay ambako gesi hiyo husafirishwa kwenda Mtwara mjini ili kuzalisha umeme unaotumika katika mikoa ya Mtwara na Lindi na nyingine hupelekwa kwenye mitambo ya kuchakata gesi ya Madimba inayomilikiwa na TPDC.

Kamati hiyo pia ilitembelea visima vya gesi vitano vilivyoko nchi kavu katika eneo hilo la Mnazi Bay, nyumba zilizounganishwa na gesi asilia kwa ajili ya kupikia na matoleo ya bomba kubwa la gesi ambayo hupeleka gesi maeneo mbalimbali ikiwamo kiwanda cha Saruji cha Dangote, mkoani Mtwara.

Wajumbe hao walitembelea mitambo ya kuchakata gesi asilia Madimba yenye uwezo wa futi za ujazo milioni 210. Gesi hiyo baada ya kuchakatwa, husafirishwa kwa bomba kubwa linalotoka eneo hilo mpaka mkoani Dar es Salaam, hivyo kuwezesha gesi hiyo kutumika kwa matumizi mbalimbali ikiwamo kuzalisha umeme, kutumika viwandani, kwenye magari na majumbani.

Vilevile, wajumbe hao walitembelea vituo vya kupokea gesi iliyochakatwa vya Somanga mkoani Lindi na Kinyerezi jijini Dar es Salaam.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga (kulia), akizungumza na wanunuzi wa madini ya dhahabu katika soko kuu la madini Kahama, mkoani Shinyanga jana, alipofanya ziara kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili ili kuzitafutia ufumbuzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wajenga nyumba ya mganga kwa mapato mazao ya misitu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KIJIJI Cha Ihombwe katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi wilayani Kilosa, kimetumia mapato ya misitu kujenga nyumba ya mganga wa zahanati ya kijiji na kunusuru uhai wa mama na mtoto kwa kuwapunguzia safari ya zaidi ya kilomita 20 kufuata huduma ya afya.

Kabla ya kujengwa kwa nyumba hiyo, wananchi walikuwa wakifuata huduma Mikumi jambo linalosababisha kinamama kujifungulia njiani na wengine kuhofiwa kupoteza maisha.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ihombwe, Vashty Chimile, alisema hayo jana wakati wa kikao cha pamoja na viongozi wa Shirika la Kuhifadhia Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) juu ya maendeleo na changamoto za usimamizi shirikishi wa misitu kwa jamii (USMJ).

Uhifadhi huo unafanyika kupitia mradi wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya misitu Tanzania (CoforEST) unaotekeleza mradi katika wilaya saba za Tanzania kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC).

Chimile alisema kabla ya mradi wa CoForEST ulioanzishwa mwaka 2019, jamii wakiwemo kinamama, hasa wajawazito saba wajifungulia njiani kwa sababu walitumia muda mwingi barabarani kwenda katika Hospitali ya Mtakatifu Kizito kupata huduma kwa sababu mganga wa zahanati alilazimika kwenda kijijini mara moja kwa wiki baada ya kukosa nyumba ya kulala.

Alisema baada ya kuchoshwa na usumbufu huo na kuona wanayo makusanyo ya mapato ya mradi, waliamua kutenga kiasi fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mganga wa zahanati, madarasa, kujenga vyoo viwili vya Shule ya Msingi Ihombwe, kuweka umeme kwenye majengo ya serikali na ukarabati wa barabara kwa kiwango cha changarawe.

Ofisa huyo alisema fedha hizo zilitokana na mapato ya mazao ya misitu zaidi ya Sh. milioni 200 ambazo walizokusanya tangu mradi unaanza hadi mwaka huu.

Mmoja wa wajumbe ya kamati ya msitu wa kijiji, Asteria Maliki, alisema kinamama wamekuwa waathirika wakubwa kiafya na kwamba anaushukuru mradi kwa kuwawezesha kupata fedha za kutosha kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Awali hatukuwa na nyumba ya mganga hapa na mama akishikwa uchungu usiku, alilazimika kujifungulia njiani na wengine wamekuwa wakifariki dunia njiani," alisema.



## Abainisha namna kufikia uchumi wa kati kwa Tanzania

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

Ili Tanzania ifike kwenye uchumi wa kati wa juu, Watanzania wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii ikiwamo kutumia fursa mbalimbali zinazowazunguka ili kujiinua kiuchumi, imeelezwa.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Aziza Mumba, wakati akifungua semina ya wajasiriamali wadogo wanaojihusisha na uzalishaji wa mvinyo mkoani hapa. Semina hiyo iliandaliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Mumba alisema serikali inaendeleza mnyororo wa thamani katika mazao mbalimbali likiwamo zabibu, hivyo wajasiriamali wanapaswa kutokata tamaa ili kukuza uchumi wa nchi.

"Nashukuru TBS kwa kufanya haya mafunzo kuwapatia ujuzi na kuwajengea uwezo ili wawe jasiri katika usindikaji wa zabibu jambo ambalo litawasaidia sana katika kuongeza kipato na kupata soko kubwa ndani na nje ya nchi," alisema Mumba.

Alizitaka halmashauri zote Mkoa wa Dodoma kuendelea kutoa ushirikiano kwa TBS wanapoendelea kutoa bidhaa zenye viwango.

Meneja wa TBS Kanda ya Kati, Nickonia Mwabuka, alisema shirika limeandaa mafunzo hayo kwa kushirikiana na SIDO lengo likiwa kuwajengea uwezo ili kuzalisha bidhaa zenye ubora na usalama hatimaye kujikwamua kiuchumi.

"TBS inasaidia kupima bidhaa hizi ili kuwa na soko la kimataifa na mpaka sasa wasindikaji 15 wamefaidika na mfumo huu na kupitia mafunzo haya, watafanikiwa kwa kiasi kikubwa "alisema Mwabuka.

Wajasiliamali walioshiriki mafunzo hayo, walisema kwao ni fursa kubwa kwa kuwa wanajifunza namna ya kuboresha bidhaa zao zinazotokana na zabibu jambo ambalo litasaidia kupata masoko na kujulikana ndani na nje ya nchi.

Ofisa Kilimo wa Jiji la Dodoma, Agness Woisso, alisema wataalamu wanasema mvinyo mzuri unaanzia shambani, hivyo ni lazima wakulima wajua ni namna gani watazalisha zabibu nzuri.

# Wizara yatafsiri sheria 154 kwa lugha ya Kiswahili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema hadi sasa wizara yake imetafsiri sheria 154 na kuzipeleka katika lugha ya Kiswahili huku akisema kazi hiyo ni endelevu.

Prof. Kabudi aliyasema hayo jijini Dodoma wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio katika sekta ya sheria kwa kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

"Kwa hiyo hadi sasa sheria 154 zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kwa hatua ya rasimu ya kwanza na kazi ya kutafsiri linaendelea. Ni matarajio yetu ndani ya miaka miwili ijayo, tutakuwa tumepiga hatua kubwa katika kutafsiri sheria.

"Kazi kubwa tuliyo nayo sasa ni kutunga kitabu cha istilahi za kisheria kwa Kiswahili ili kusiwe na tafsiri za mitaani katika kutafsiri maneno ya kisheria ya Kingereza. Haya yote ni mafanikio makubwa sana," alisema Prof. Kabudi.

Kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mahakama, alisema katika kipindi chote mahakama za mwanzo hadi za rufani, Kiswahili kimekuwa kikitumika.

"Kanuni za Mahakama ya Rufani zilizopitishwa wakati wa Jaji Mkuu Augustino Ramadhani, ziliruhusu matumizi ya Kiswahili. Kwa hiyo katika Mahakama za Mwanzo, Kiswahili daima kimekuwa kikitumika na katika Mahakama ya Rufani wewe unayepeleka shauri ulikuwa na hiari kutumia Kiswahili au Kingereza," alisema.

Pia alisema katika maeneno ambayo bado Kingereza kilikuwa kinatumika, ni katika Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu.

Alisema utungaji wa sheria zote ulifanyika kwa Kingereza lakini pia ziko sheria ambazo zilipotungwa, zenyewe zilisema mara baada ya sheria hii kutungwa zitafsiriwe kwa Kiswahili ambazo ni Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

"Kwa hiyo uamuzi uliofanywa ya mabadiliko ya sheria mwaka jana ni kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kutunga sheria. Maana yake sasa sheria zitatungwa na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili," alisisitiza

Prof. Kabudi alisema mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuwa na taifa lililoingia katika uchumi wa kati miaka mitano kabla ya muda uliokadiriwa na katika kipindi kigumu cha mlipuko wa janga la corona.



Meneja Mauzo na Bwanashamba wa kampuni ya Yara Tanzania Ltd, Andrew Mwangomile, akizungumza na wakulima wa zao la zabibu Mkoa wa Dodoma, wakati wa mafunzo ya kilimo cha zao hilo, yaliyoandaliwa na kampuni ya Tanzania Breweries Ltd, wilayani Chamwino juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanachama SACCOS waonya matumizi mikopo

**Na Renatha Msungu,**DODOMA

KATIBU MKuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Christopher Kadio, amewataka wanachama wa SACCOS ya Tanzani Prison Services (TPS) iliyo chini ya Jeshi la Magereza kutumia mikopo wanayopewa kwa ajili ya kuzalisha mali na kuacha kutumia fedha kwa mambo yasiyo na tija.

Kadio aliyasema juzi jijini Dodoma wakati wa ufunguzi wa mkutano wa tisa wa SACCOS ya TPS, uliofanyika kwa lengo la kuiboresha ili watu wakope.

Alisema fedha za mikopo ambazo wanazipata ni vyema zikatumika kwa ajili ya kuzalisha mali na kujiinua kiuchumi kwa kufanya biashara mbalimbali.

"Dhana ya SACCOS ni uzalishaji mali na si kutumia pesa mnazokopa kwa ajili ya kufanya starehe ikiwamo kununua gari kama Toyota V8, PRADO na nyinginezo," alisema Kadio.

Pia aliutaka uongozi wa bodi kufanya ushawishi ili kuwahimiza wafanyakazi kujiunga na chama hicho kwa kuwa kinaonekana kuwa kina tija kubwa kwa wafanyakazi wake.

Alisema binafsi amenufaika kwa kukopa fedha ndani ya SACCOS ambazo amezifanyia mambo makubwa ya kimaendeleo, hivyo kuna kila sababu ya kuwashawishi wafanyakazi wote kujiunga.

"Ili chama kiwe kizuri ni lazima kiwe na kipaumbele lakini pia lazima kizingatie sheria na taratibu kwani mambo hayo yakizingatiwa, SACCOS itakuwa kubwa zaidi," alsema Kadio.

Katibu Mkuu alisisitiza elimu ya ushirika izidi kutolewa, ikiwamo kujua masharti yaliyopo pamoja kufanya usimamizi ulio sahihi na kwamba hilo viongozi wanapaswa kulizingatia.

Aliwataka wanachama katika warsha hiyo kutoa maoni ya msingi ambayo yataijenga saccos hiyo na si kuibomoa.

Akitoa neno la shukrani, Makamu Mwenyekiti wa Bodi, Mzee Nyamka, ambaye ni Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza, alisema wanatambua kuwa jukumu lao kubwa ni uzalishaji mali pamoja na kutoa elimu ndani ya chama ili wanachama wawe na uwelewa.

Nyamka alisema wamekuwa wakihimiza uaminifu kwa wanachama wao pamoja na viongozi ili kuhakikisha chama hiko kinakuwa na wanachama ambao ni waaminifu.





# Ongezeko magonjwa akili yamshtua Rais Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, amesema magonjwa ya akili ni changamoto kubwa kwa nchi zote duniani na kwamba takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa kila penye watu wanne, mtu mmoja ana uwezekano wa kupata ugonjwa huo maishani mwake.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika hafla ya ufunguzi wa jengo jipya la Hospitali ya wagonjwa wa akili, Kidongochekundu mjini Zanzibar, lililojengwa kwa ushirkiano kati ya Serikali ya Zanzibar na wafadhili kutoka Norway.

Alisema kwa Zanzibar maradhi hayo yanawasibu wananchi kadhaa na kuanzia mwaka 2000 hadi 2020, watu wapatao 18,595 wenye maradhi ya akili walisajiliwa. Alisema kiwango hicho ni kikubwa na kinaonyesha umuhimu wa kuwapo mpango mkakati mahsusi ya kupunguza kasi ya ugonjwa huo.

Dk. Mwinyi alisema si kila wakati maradhi hayo yanatokana na vinasaba na urithi wa kibaiolojia kutoka kwa wazazi, bali kwa baadhi ya wakati, maradhi hayo yanatokana na mabadiliko ya mitindo ya maisha.

Alisisitiza kuwa ni vyema kuimarisha utamaduni wa kusaidiana, kupendana, kuliwazana na kufarijiana wakati wa shida na misukosuko ya kimaisha.

"Tuendeleze utamaduni wetu wa asili wa kutembeleana na kujumuika pamoja katika shughuli mbalimbali ili kupunguza msongo wa mawazo na kuishi tukiwa katika furaha. Tuimarishe malezi ya watoto na vijana ili kujiepusha na mambo ambayo huathiri afya na mwelekeo wao wa maisha," alisema.

Dk. Mwinyi alisema zinatakiwa nguvu za ziada kupambana na uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya, tatizo ambalo linachangia kuvuruga, kuchanganya na kuharibu akili za watoto na vijana.

Pia alisema alisema haridhishwi na utaratibu na usimamizi wa utoaji huduma wa dawa ya 'Methodone' ambayo hutumika kuwasaidia wagonjwa wa dawa za kulevya ili waache matumizi ya dawa hizo na kuishi maisha ya kawaida ambayo huduma hiyo hutolewa hapo Kidengochekundu.

Alisema kuna kasoro nyingi za ufuatiliaji wa maendeleo na tiba za wanaopatiwa huduma na hakuna utaratibu mzuri wa kutathmini mabadiliko ya tabia kwa waathirika wanaopatiwa huduma hiyo pamoja na mambo wanayoyofanya wakiondoka kituoni hapo.

"Isifike mahali kitengo hiki kikageuzwa kuwa kijiwe cha kukutanisha makundi mbalimbali ya wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevya na isifike mahali waathirika wakaona kwamba kazi ya kituo ni kuwapatia huduma kwa ajili ya kubadilisha hisia za uraibu pale wanapokosa fedha za kununua dawa za kulevya na si kutafuta tiba ya kudumu," alisema.

Dk. Mwinyi alisema amepata taarifa ya kuwapo manung'uniko kutoka kwa wakazi wa eneo hilo na maeneo jirani juu ya ongezeko la vitendo vya uhalifu vinavyofanywa na baadhi ya waathirika wa dawa za kulevya wanaofika hapo kutafuta tiba.

Alisema baadhi ya vijana hao hawafuati utaratibu uliopo badala yake huzurura ovyo jambo ambalo ni tishio kubwa kwa usalama wananchi na mali zao. Rais aliuagiza uongozi wa wizara ya afya na wakala wa uthibiti wa dawa za kulevya kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo zinazohusu mfumo mzima wa utoaji wa huduma wa Methodone na kuharakisha ujenzi wa kituo cha kurekebisha tabia kwa waathirika huko Kidimni, Unguja na Kangagani, Pemba.

Naye Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema wizara inaendelea na juhudi za kuhakikisha afya za wananchi wa Zanzibar zinaimarika na kuwa bora.

Alisema katika kipindi kifupi kijacho, wizara hiyo itaipatia vifaa vya uchunguzi hospitali hiyo ili kuwaondolea usumbufu wagonjwa wanaofika kufuata tiba, lengo likiwa ni kuondoa changamoto zote zinazoikabili sekta ya afya.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mwenyekiti wa UBA Bank Group, Tony Elumelu, alipomtembelea Ikulu, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Elumelu aliahidi kuendelea kuunga mkono miradi mbalimbali ya serikali kwa ajili ya kuendelea kuinua uchumi wa Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uongozi chuo wafariji wafiwa, majeruhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Chuo Kikuu cha Bugema nchini Uganda, umefika Zanzibar kuwafariji majeruhi wa ajali ya basi pamoja na familia za waliopoteza ndugu zao ambao walifariki dunia kutokana na ajali mbaya ya gari iliyotokea uni 2, mwaka huu, mjini Shinyanga.

Ajali hiyo ya basi la abiria lilikuwa limebeba wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Bugema waliokuwa wakirejea nchini Tanzania.

Akizungumza jana na uongozi wa chuo hicho, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abbdulla, aliupongeza uongozi wa chuo kwa kufika Zanzibar kuwaona wanafunzi waliojeruhiwa kutokana na ajali hiyo.

Alisema serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya, inaendelea kuwahudumia kwa karibu wale wote waliopata ajali iliyosababisha majeraha na wengine kupoteza viungo ili kuimarisha afya zao.

Hemed alisema serikali itaendelea kuwahudumia waathirika hao kwa lengo la kuziimarisha afya zao ili waendelee na majukumu yao katika kulitumikia taifa.

Aidha, Hemed aliuhakikishia uongozi wa chuo hicho kwamba serikali itaendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha azma iliyokusudiwa ya kuwatayarisha wanafunzi kuwa wataalamu bora kupitia kada ya afya inafikiwa.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Paul Katamba, alisema uongozi wa chuo umeamua kufika Zanzibar kwa lengo la kuziona na kuzifariji familia za majeruhi pamoja na wafiwa.

Alisema majeruhi wa ajali waliokio Zanzibar kwa sasa chuo kimeamua kuja na utaratibu maalum wa masomo wa kutumia njia ya mtandao ambao utawawezesha kumalizia masomo yao wakiwa Zanzibar.

# Waziri asisitiza kutunza mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwaza wa Rais Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema kuna umuhimu mkubwa katika kuyatunza na kuyahifadhi mazingira ili kuhakikisha ardhi inarudi katika hali ya ubora na kupunguza maafa.

Mkuya aliyasema hayo jana huko Maruhubi katika Ofisi ya Idara ya Mazingira alipokutana na Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia ofisi ya viongozi wakuu wa kitaifa.

Alisema hali ya mazingira ya Zanzibar kiujumla hairidhishi kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi pamoja na uharibifu wa mazingira kwa sababu ya uchimbaji holela wa mchanga, ukataji miti ovyo na kuzagaa plastiki chafu.

Alisema hali hiyo imefanya baadhi ya maeneo kuwa katika hali hatarishi na kusababisha mmomonyoko wa udongo, kutuwama maji kwa wingi na kusababisha maji ya bahari kupanda juu kwa kina kikubwa.

Kwa mujibu wa Mkuya, hali hiyo lazima irekebishwe kwa kupanda miti kwa wingi, kuchimba mchanga kwa kufuata maelekezo ya kitaalamu ili kuinusuru nchi na maafa yasiweze kutokea.

Alisema katika kupambana na hilo serikali italazimika kujipanga zaidi ili kuyanusuru mazingira ya Zanzibar na kwamba katika kikao kijacho cha Baraza la Wawakilishi, serikali itatoa tamko rasmi kuhusu mazingira Zanzibar.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayosimamiaa ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa, Mtumwa Peya Yussuf, alisema kutokana na hali ya kuharibika mazingira, Zanzibar italazimika kupanda miti kwa wingi ili kuirejesha ardhi katika asili yake.

Alisema mchanga utalazimika kuchimbwa kwa kufuata maelekezo ya kitaalam, miti isikatwe ovyo, mifuko idhibitiwe kwa sababu bado inaingizwa nchini na kuweka mikakati kwa waekezaji wanaowekeza katika visiwa na maeneo mengine ili kuvituza visiwa hivyo.

BASI SAWA

## Babalevo umeyasikia ya Oti?

ALIYEKUWA msanii wa Babalevo, anayefahamika kama Oti, ametibua hali ya hewa baada ya kudai kunyanyaswa na msanii huyo ikiwamo kupigwa.



Oti, akizungumza na Bongo5 amesema maisha akiwa na babalevo yalikuwa magumu kiasi ambacho amepoteza ndoto yake ya kuwa mwanamuziki mkubwa.

"Ameniharibia maisha yangu, Rayvanny alitaka kunisaidia akamshambulia na maneno mtandaoni, nipo katika mchakato wa kujiondoa rasmi na tayari nimewasiliana na mwanasheria kuvunja mkataba ili niweze kufungua kesi ya madai," amesema.

## Rayvann kanogewa Colombia

BAADA ya kufanya vizuri katoka usiku wa tuzo za MTV EMA, sasa mkali wa Bongo Fleva, Rayvann na mwanamuziki toka Colombia, Maluma, wanatarajia kutoa ngoma yao mpya hivi karibuni.

Katika ngoma hiyo ambayo kionjo chake kimetoka wiki hii, amesikika Rayvann akiimba kwa lugha ya Kihispania jambo ambalo limeibua mjadala mkali kuhusu wimbo huo.

Malema atakuwa mwanamuziki wa kwanza kuimba nyimbo mbili na mwanamuziki huyo kutoka lebo ya WBC, wimbo wa kwanza waliofanya kazi pamoja ni ule 'Mama Tetema' ambao waliurudia.





## Marioo kama umelewa bia

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya, Marioo, ameamua kumwaga ugali kwa kuwakabili wababe wa muziki huo nchini, kwa kuwaita malimbukeni wa wanamuziki chipukizi kutoka nje.

Akizungumza bila kutaja majina kupitia ukurasa wake wa Instagram, Mario amesema anaumia kuona wasanii hao wakongwe wanawachukua wanamuziki wachanga kutoka Nigeria na Afrika kusini na kuwaacha hapa nchini wakisota.

Mwimbaji huyo wa 'Bia Tamu'amewataka kuacha tabia ya kumsubiri Rais Samia Suluhu Hassan, azungumze kwani watakuwa wanachelewa.





## Flaviana pole kwa yaliyokukuta

MWANAMITINDO Flaviana Matata, amewaonya watu wanaowasakama mastaa ambao wametalikiana na wenza wao.

Amsema amefurahishwa na kitendo cha Mwimbaji wa wa Uingereza Adele, kuweka wazi kuhusu talaka yake, lakini alisema baadhi ya watu wanashambulia bila huruma endapo kuna tatizo la kupeana talaka.

"Uuzoefu wangu wa binafsi nilitalikiana mwaka 2019, watu na mtandao ya kijamii hawakuniruhusu kupumua, ilikuwa kana kwamba nimeua mtu" amesema Flaviana Matata.

## WA-MAMA WALIOPAGAWISHA WABONGO

**Na Adam Fungamwango**

MIAKA ya 1970, 1980 mpaka mwishoni mwa miaka ya 1990 ilikuwa si kilele cha mafanikio ya muziki si Tanzania tu, bali hata nje ya nchi.

Wanamuziki kutoka Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Afrika Kusini walitoa nyimbo kadhaa ambazo zilikuwa na mashabiki wengi nchini Tanzania.

Kati ya hao walikuwa wanamuziki wa kike ambao hawakuwa nyuma, kwani walitikisa na nyimbo zao kupenya na kuvuka mipaka ya nchi zao hadi Bongo, zikikubalika na kuwachengua mashabiki wengi wa muziki wa dansi.

Leo tutawaangalia baadhi ya wanamzuki wao, pamoja na nyimbo zao ambazo zilitikisa kila kona ya nchi na hazikukosekana kupishwa kwenye sherehe mbalimbali za kijamii kama vile harusi, ubatizo, kipaimara, hata za kiserikali.

**Mbilia Bel**

Ni mwanamuziki wa kike Mkongomani, aliyekuwa kwenye kundi ya Africa Intenational chini ya Tabu Ley. Mbilia Bel pia alikuwa mke wa Tabu Ley na walijaaliwa kupata mtoto mmoja wa kike.

Alitunga na kuimba nyimbo mbalimbali ambazo zilimpatia umaarufu mkubwa duniani kote kuanzia miaka ya 1980. Hapa Tanzania nyimbo zake zilizopendwa mno ni 'Nakei Nairobi' na 'Nadina'.

**Yondo Sister**

Kwa hakika huyu alipendwa mno na mashabiki wa muziki Tanzania na ndiye maarufu zaidi kutokana na aina yake ya muziki ya soukouss. Aliibuka mwanzoni mwa miaka ya 1990. Kilichompatia umaarufu zaidi Mkongomani huyu si kuimba tu, bali pia kucheza. Alikuwa na uwezo wa kucheza kama mtoto wa kike, lakini wakati mwingine kama mwanamume, huku pia akiwa amepigilia mavazi ya kiume kama vile jeans lililopasuliwa. Ni mmoja wa wanamuziki walioingiza fasheni ya majinzi kuchwanwa na yenye kupauka. Pia kwa wanawake alileta fasheni ya msuko wa nywele ambao uliitwa 'Yondo Sister'. Na hii ilitokana na aina ya nywele alizosuka kwenye 'kava' na albamu ya 'Deviation', inayoonekana kwenye picha ya makala hii.

Nyimbo zilizompatia umaarufu ni 'Wapi Yo', 'Bazo', 'Deviation', 'Mwana Kento', na nyingine nyingi.

**Tshala Muana**

Huyu ni mwanamuziki mwingine wa kike mkongwe wa Kikongomani, mwenye vituko vingi ambaye anakumbukwa na Watanzania kutokana na ziara zake nyingi alizokuwa akizifanya Bongo na kuacha simulizi.

Pamoja na nyimbo nyingi alizoimba kwenye lugha ya 'kiluba', moja ya kabisa maarufu nchini Congo DR, Tshala Muana alikuwa na mashabiki wengi kutokana na kuimba nyimbo nyingi kwa lugha ya kiswahili kama 'Dezo Dezo', 'Sitambili', 'Karibu Yangu', pamoja na ule wa 'kiluba' ulitwao 'Kokola'.

**Yvonne Chakachaka**

Huyu ni mwanamuziki wa kike kutokea nchini Afrika Kusini. Alianza kutamba mwanzoni mwa miaka ya 1980 hadi mwishoni mwa 1990. Nyimbo maarufu ambazo ziliwapagaiwsha Wabongo ni 'Umqombothi', 'Sangoma', 'Thank you Mr Dj', 'Stemela' na nyingine nyingi.

**Brenda Fassie**

Ni mwanamuziki wa Kisauzi aliyefariki mwaka 2004. Aliwahi kufanya ziara nchini Tanzania na akatamba sana na ngoma yake ya 'Vulindela'.




## Binamu: Mzaha mzaha hutumbuka usaha

**Na Adam Fungamwango**

PENZI halichezewi na wala halijaribiwi. Ndivyo unavyoweza kusema. Ni msemo wa wahenga tangu enzi na enzi. 'Binamu' ni filamu iliyochezwa na wasanii Affan Jamal, Diana James, Ahur James, Jumanne Simba na wengine. Ni filamu inayotoa funzo kwa watu kuwa waangalifu sana wanapokuwa kwenye uhusiano au ndoa.

Usimfanyie kitu mpenzi wako ambacho wewe hutaki kufanyiwa. Kwa sababu ipo siku unakuja kufanyiwa wewe ukakasirika.

Jamaa mmoja anaitwa Sharukhan. Huyu ana mkewe Zaina. Kwa sababu wamekaa muda mrefu bila ya kuwa na mtoto, Sharukhan anamwambia mkewe amelete dada yake binamu ili angalau nyumba ichangamke. Analetwa dada mmoja anaitwa Ashura. Ni Ashura, Ashura kweli. Kipande cha dada, kimeumbika.

Siku si nyingi, mke wa Sharukhan akaanza kuona kama mwenendo wao siyo mzuri. Walionekana ni kama wapenzi hivi. Mara kwa mara akawa wanawakuta wanadekezana na kukumbatiana. Zaina anapoulizwa akaambiwa kuwa hiyo ndiyo tabia yao tangu utotoni kwa sababu wamekuwa pamoja.

Hali hiyo ilimfanya Zaina asipate usingizi. Akawaza na kuwazua. Iko siku na yeye akakata shauri ya kumpigia kaka yake binamu aje. Sharukhan akafungwa kamba kuwa kaka wa mkewe anakuja kusalimia. Lakini lengo ilikuwa ni kulipiza kisasi.

Anakuja kaka yake. Kinachotokea ni kama kile ambacho Sharukhan na Ashura wanafanya. Majirani wanaona kila kitu. Na kwa bahati nzuri au mbaya, Zaina na kaka yake wanacheza ngoma, kuimba na kukumbatiana hadharani. Sharukhan anaambiwa yote. Mapenzi yanauma. Hali ya jamaa ilianza kubadilika. Sasa hata dada yake binamu, akitaka kudekezana, Sharukhan hataki. Akili yote ni kwa mkewe akiona kabisa sasa anaibiwa.

Akaitisha kikao. Akaanza kutoa kilicho moyoni mwake. Mkewe akasema amefanya vile kwa sababu ya kulipa kisasi cha



kile ambacho anafanyiwa ndani ya nyumba hiyo.

Alivyoona haelewi, maana Ashura dada si dada, basi akaona na yeye akamlete kaka yake binamu kwa ajili ya kuigiza kama wanavyofanya mumewe na Ashura ili kuweka mambo sawa. Akamwambia mumewe kuwa hata yeye alikuwa anaumia sana kwa alivyokuwa anafanyiwa.

Mwisho wa siku, kaka binamu wa Zaina ilibidi arudishwe kwao, Ashura akatafutiwa mchumba ambaye ni rafiki wa Sharukhan, yeye mwenyewe akabaki na mkewe.

# Burna Boy tambua serikali ina mkono mrefu



MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Burna Boy, ameicharukia serikali akisema kilichofanywa na kikosi cha kuzuia uhalifu (lekki) hakiwezi kufutika.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, mwimbaji huyo alikuwa akishiriki mazungumzo na mashabiki wake, na kueleza hakuna damu ya wanyonge iliyomwagika ikafutwa na uongo wa mtu mmoja.

"Wakati nimelala niliamshwa na taarifa ya serikali ya kufuta madhambi yao, nasema huwezi kufuta damu ya wanyonge kwa uongo wa mtu mmoja," amesema.



## Shyngle usiwalishe sumu wenzio

MWIGIZAJI kutoka Ghana, Princess Shyngle, ametoa ushauri kwa wanawake walioolewa nini cha kufanya pale wanapotaka kutoka nje ya ndoa yao kudanga.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Princess Shyngle, amesema wanaume wajanja sana kwani kila unapotaka kufanya jambo anajua kabla ya mwenyewe hujafahamu.


"kama umeolewa na unataka kutoka nje ya ndoa kila mara fahamu hata mume wako anatoka na wanawake wengine, nakuahidi mwanamume aliyeoa anajua kila kitu kabla yako," amesema

## Adele asifia penzi jipya

NYOTA wa muziki kutoka Uingereza, Adele, amefichua kwamba uhusiano wake na Rich Paul, umekuwa bora zaidi kuwahi kuwa nao katika anga la mapenzi.

Adele amesema hayo katika mahojiano na alieleza jinsi kupewa talaka na mume wake na uamuzi wake wa kuhamia Los Angeles nchini Marekani na mtoto wake.

Amesema "Uhusiano wangu na Paul ni wa ajabu zaidi, unatoka moyoni, wazi na rahisi"





## Duh! Haijawai kutokea

MWANAMITINDO Paris Hilton, hatimaye ameolewa tena na Carter Reum, katika harusi inayoelezewa kwamba ya kifahari.

Kulingana na mtandao wa page Six, harusi hiyo ya aina yake ilifanyika ndani ya jumba la kifahari la babu yake linaloitwa Bel-Air, siku ya Ijumaa iliyopita huko Santa Monica.

Harusi hiyo ilidhuhuriwa na wasanii na mastaa mbalimbali, marafiki na ndugu wa pande zote mbili, huku burudani ilitumbizwa na msanii nguli Paula Abdul.

## Paul Rudd usiwapagawishe wanawake

MWIGIZAJI wa Marekani, Paul Rudd, anatajwa ndiye mwanaMume mwenye mvuto wa kimahaba zaidi mwaka 2021.

Kulingana na jarida la People, msanii huyo mwenye umri wa miaka 52 ametajwa kuwa mwenye mvuto zaidi kati ya wanaume waliotakiwa kupigiwa kura.

"Ninapojifikiria mimi binafsi, najiona kama mume na baba, napenda kuwa hivyo, napenda kuwa pamoja na familia yangu na huwa sipendi kutembea hovyo," amesema wakati akizungumzia suala hlo.



MAKALA

# GABRIEL ZAKARIA
# Miezi mitano ya DC mwanahabari anayeihuisha Busega katika mapato

- Adhamiria kilimo, kufuta hesabu chafu
- Kujitosa shamba lake, uandishi palepale

**Na Anthony Gervas**, BUSEGA

JUNI 19, 2021 itabaki siku ya kumbukumbu kwake na familia, Gabriel Zakaria alipoteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Mkuu wa Wilaya ya Busega mkoani Simiyu na akaapishwa rasmi siku mbili baadaye, Juni 21.

Anakiri mbali na kumshangaza. Ikawa ndio mwanzo wake kuhama kutoka utangazaji katika Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) jijini Dar-es Salaam, kuhamia uongozi wa serikalini

Gabriel anasema katika jukumu analotumikia sasa, anaahidi kuhakikisha anatimiza ndoto za wana -Busega katika namna ya kumrejeshea Rais ujumbe wa shukrani na ishara vijana wanaweza wakipewa nafasi.

Anaieleza wilaya Busega ina fursa nyingi na za kutosha, akitaja mifani ya kilimo, ufugaji, uvuvi, madini, pia ni lango la kuingilia watalii wanapoenda hifadhini Serengeti, hivyo yeye anaamini atafanya kazi kwa vitendo na siyo maneno.



Stendi ya mabasi Nyashimo wilayani Busega. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

### VIPAUMBELE VYAKE

Zakaria anasema vipaumbele vyake ni makusanyo ya mapato, kwa sababu wakati anakabidhiwa wilaya hiyo ilikuwa ya 176 katika ukusanyaji mapato kati ya halmashauri za wilaya 184 nchini, wakinusurika kushika mkia.

Anasema amepambana kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kuhakikisha wanavuka malengo kukusanya mapato kwa mwaka uliopo wa fedha.

"Vipaumble vyangu ni makusanyo, makusanyo, makusanyo ya mapato. Mpango mkakati wa makusanyo ya ndani katika wilaya ya Busega ni kuwa ndani ya kumi bora kwenye halmashauri zote nchini," anasisitiza Zakaria.

Anafafanua kwamba mapato ndio yanampa kujenga vyumba vya madarasa, kupata fedha za maendeleo, hata asilimia 10 ya kugawia vijana,wanawake,wenye ulemavu wala kuboresha miundombinu ya barabara, afya na maji.

Kwa mujibu wa Zakaria, hivi sasa makusanyo ya robo ya kwanza; miezi Julai, Agosti na Septemba katika mwaka wa fedha uliopo wamefanikiwa kukusanya ya asimilia 100 ya malengo.

Anaeleza kuwa, serikali imewapangia kukusanya Sh. milioni 486 katika miezi mitatu na kwa mwaka kukusanya Sh. bilioni 1.7, ili kufikia lengo la kukusanya bilioni 1.9 mkuu wa wilaya anafafanua wamevuka lengo la Sh. Milioni 486 kwa miezi mitatu, wakikusanya Sh. milioni 500.

Pia, Zakaria anaifafanua Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Mwaka 2019/20, inaonyesha wilaya ina asilimia 'sifuri'katika kuchangia asilimia 40 ya fedha za maendeleo.

Makusanyo ya madini yalikuwa nyuma, lakini hivi sasa wanakusanya hadi Sh. milioni 10 kila mwezi kutokana na kuuza viroba, wakiwajibika na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Busega.



Mkuu wa Wilaya ya Busega, Gabriel Zakaria, akiwa ofisini kwake.

### PENYE KILIMO

Mkuu wa Wilaya Zakaria, anasema hivi sasa mkakati mkubwa alio nao ni wakulima wa pamba kwa wingi msimu huu, bei yake kilo moja ni Sh. 1,900, ambayo haijawahi kufikiwa tangu kupatikana Uhuru wa nchi, pia kusambazwa mbegu bora kwa wakulima, akiwahimiza kutumia mbinu za kisasa, kwa malengo ekari moja itoe zaidi ya kilo 1000.

Aidha, anasema wanatarajia kuzalisha pamba tani 500,000 kutoka tani 200,000 akiahidi binafsi naye anajitosa kulima pamba ekari 50, kufuga nyuki mizinga 100, zao la alizeti ekari 20 pamoja na shamba la pilipili.

Hapo anaweka msisitizo kwamba, zao la asali nalo lina faida kubwa, kwani lita moja ya asali bero yake ni Sh. 15,000.

Jingine analolihimiza ni kampeni ya upandaji miti wilaya nzima, akiamini ni kampeni itakayokuwa na manufaa makubwa kwa wakazi wa Busega, ikiwamo kuwahimiza kupanda miti ya matunda, lengo ni kuiona Busega 'ya kijani'.

### MAGUMU YALIYOKO

Anasema tangu aanze kuchapa kazi wilayani humo ametimiza wastani wa miezi mitano na anaguswa na magumu yaliyoko mahali, akiahidi kufunga mkanda na wenzake kuzitatua.

Shida mojawapo aliyokutana nayo ni kukosekana stendi ya mabasi Nyashimo, ambayo ni kilio kikubwa cha wakazi, ila sasa inaendelea kujengwa, huku ikitoa huduma za wasafiri kwa wananchi katikia kiwango chake duni.

"Siku moja nikipita, nilizuiliwa barabarani na wananchi wakifunga barabara. Kilio chao kikubwa wanataka kujengewa kituo cha mabasi, kwamba wamechoshwa na ajali za barabarani. Bila kusubiri nilianza na kero hiyo kuitatua," anaeleza Zakaria.

Anataja la pili, hakuna Mahakama ya Wilaya, ingawa hivi sasa tayari imeshaanza kujengwa, lakini wananchi bado wanalazimika kwenda kupata huduma katika wilaya jirani.

Vilevile, anagusa kutokuwapo hospitali ya wilaya na kuna kero ya ukosefu wa majokofu ya kuhifadhi maiti katika maendeleo ya tiba, hata inawalazimu wananchi kusafirisha maiti kwa gharama kubwa kwenda kupata huduma wilayani Magu, mkoa wa Mwanza.

Hiyo anaitaja na kero zingine alizokumbana nazo ni pamoja na Wilaya kutokuwa na Soko, Dampo, eneo la Makaburi, huduma za maji bomba na barabara, ambazo zinaendeleo kushughulikiwa ikiwamo kutenga eneo la wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga.

Kabla ya kujengwa stendi ya mabasi, halmashauri ya wilaya hiyo ilikuwa ikipoteza kodi ya mabasi makubwa na magari madogo aina ya Hiace na Mchomoko, yaliyokuwa hayaingii stendi kila siku, akiweka takwimu mabasi 180 hadi 190, michomoko nane hadi 10 na Hiace kati ya 20 hadi 25.

Mkuu wa Wilaya anaeleza dhamira yake kuhusu mvutano wa ujenzi wa stendi ya mabasi katika mji wa Lamadi, uliogubikwa na masuala ya kisiasa kwa takribani miaka saba, atahakikisha anasimamia ujenzi wake kumaliza mvutano ulioko.

### MPANGO MIKAKATI

Mkuu wa Wilaya anaangalia pia eneo la wanawake na vijana waweze kutengeneza vitu vya asili kama vile vya kitamaduni, ili kudumisha mila na utamaduni za kabila la Wasukuma, ili kuvutia watalii wanaofika hapo safari kwenda Serengeti.

Daima Zakaria, licha kuhama kiti chake cha uanahabari, bado anaazimia kutouacha uandishi wa habari maisha yake yote, akiwa nje ya muda wa kazi, hata kama atakoma ukuu wa wilaya.

Katika eneo hilo anagusa katika dhamira anayoieleza kuanzisha televisheni ya 'online', akitaja ya kipekee kwa ajili ya kuleta mapinduzi kwenye teknolojia ya utangazaji.

**Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa barua pepe; anthonygervas@yahoo.com na simu:+255 682 86 92 44.**

MAKALA

## TUNAKOTOKA, TULIPO NA TUNAPOELEKEA...

# Kutoka zama mshahara Sh.380, ada Sh. 4,000 shule 'babu kubwa'

Na Adam Fungamwango




JAMANI pesa hii inashangaza kidogo! Mtu akitajiwa thamani au bei ya kitu wakati huo, leo hii anaweza kubaki katika mshangao hata kuhisi ni masihara. Ndio maisha na lazima yaendelee!

Ebu tafakari hili la zama hizo katikati ya miaka 1970, katika basi jipya mali ya Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) aina mpya Leyland CD wakati huo ikiwa katika 'chati'; mbele ya usukani wa dereva kuna angalizo: "Tahadhari; endesha kwa uangalifu imenunuliwa nusu milioni."

Leo hii ni thamani iliyoko mtaa mmoja na kima cha chini cha mshahara au beu ya simu ya mkononi ya kawaida sana. Vivyo hivyo katika kipindi cha sasa, wanafunzi wakiwa katika mchakato kujiunga na kidato cha kwanza kwa shule binafsi, wengi ada si chini ya Sh. 800,000 kusonga Sh. milioni moja na ushee hadi milioni kadhaa kwa bweni, hata kuzua ulinganishi unaokuacha mdomo wazi.

Sehemu ya fomu ya kujiunga kidato cha kwanza kwa shule inayogombewa zama mwanzoni mwa miaka ya 1980 yenyewe inasomeka:"Kutokana na kuongezeka gharama za mahitaji, ada sasa itakuwa Sh. 4,140 kwa wanafunzi wa bweni".

Kuna mengi ziadi ya hapo. Viatu vyeupe raba 'AS' maarufu 'Asante Salim' kutokana na Waziri Mkuu wa wakati huo, Salim Ahmed Salim ziliuzwa Sh. 100, huku raba nyeupe ambazo kiasi fulani inafanana na hizo 'AS'.

Pia, kabla ya hapo miaka ya 1970 maarufu 'raba mtoni' ilionekana kuwa na bei inayotisha, Sh. 300, mvaaji akiringa na kuvijali kupitiliza, hathubutu kamwe walau kupiga navyo mpira.

Hapo ndipo mwishoni mwa miaka ya 1970 viatu virefu aina ya raizoni kama zilizotolewa picha yake Jumamosi iliyopita zilishuhudiwa kutikisa kwa bei ngazi nne ikiuzwa Sh. 450; ngazi tatu Sh. 380; ngazi mbili Sh. 250, huku viatu maarufu za mikanda vya plastiki 'chachacha' au 'saa sita utanikoma' viliuzwa Sh. 13.



Sasa rejea wavaaji raizoni hawa wanaoonekana 'mabitoz' wa bei mbaya mishahara yao ikoje, zama hizo utitiri wa viwanda kila kona? Kwa mujibu wa viwango rasmi vya malipo ya umma vilivyosimamiwa na shirika maarufu lililokuwapo SCOPO, mshahara kima cha chini Sh. 380.

Hapo kuna waajiri kama kiwanda cha viatu bora walilipwa kima cha chini Sh. 450 hata waajiriwa wake kuonekana wako juu kimaisha.

Ikikumbukwa mabasi binafsi yanayoiba 'ruti' hayana leseni yalikuwa nauli Sh. tano hata kubatizwa jina 'daladala', tofauti na walio halali UDA Sh. tatu na senti hamsini, kwa nauli ya mwanzoni mwa miaka 1980

Shuleni kuanzia miaka ya 1970, wanafunzi wamepewa hela ya matumizi senti tano hadi kupanda senti 10, senti 20 maarufu 'mbuni' zikiwa na nguvu ya kuweka mambo sawa kununua muhogo wa kuchoma au kuchemsha au ile maarufu zaidi ya kukaanga, kachumbari na 'mazagazaga' mengineyo mtoto akashinda shuleni salama tumboni.

Katika mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mujibu wa sheria kila mwisho wa mwezi vijana walilipwa posho maarufu 'kichele' Sh. 300 kiwango kilichodumu hadi mwanzoni mwa mwaka 1990.

Ni 'maajabu na kweli' pesa hizo zilitosha hata vijana hao wakijidai mwisho wa mwezi kwenda kujinasibu kimatumizi na marafiki na baadhi wapenzi kambini, katika sehemu kwenye biashara za kutimia maarufu 'vibanda hasara' pesa zikitosha mahitaji yao na baadhi walibana matumizi kujibana tayari kwenda kuanza maisha.

Kwa wale wa jijini Dar es Salaam watu wa 'matanuzi' kwamba miaka ya 1980, kumbi za starehe hasa za sinema na muziki kiingilio kilikuwa ni Sh. saba, hadi 12 kutegemea na ukumbi wenyewe ambao mtu anataka kwenda kuangalia sinema.

Kwenye miaka hiyo hiyo, kiingilio kwenye dansi kilikuwa Sh. hamsini kwa wakubwa na itakumbukwa miaka ya 1980 hadi mwishoni mwa 1990, kulirudishwa dansi za jioni kuanzia saa 10 hadi saa 4:00 usiku, hasa siku za Jumapili na yote ni kwa sababu kesho yake Jumatatu watu wawahi kazini.

Hiyo ilisababisha hata watoto nao chini ya miaka 18 kuanza kuingia dansini mchana, lakini mwisho wao ilikuwa ni saa 12:00 jioni au saa 1:00 usiku wanatakiwa wawe wameshatoka nje kurudi makwao. Kiingilia chao kilikuwa Sh. ishirini.

Mtu anaweza ukaiona jinsi pesa ndogo, lakini kwa wakati huo ilikuwa 'mbinde' kuipata, watoto waliokuwa damu ya muziki, au wanaopenda muziki walilazimika kubania pesa wanazopewa kwenda shule ili kuweza kupata kiingilio, pia zile wanazopewa na watu wengine wananunue biskuti, koni au peremende.

Wala haikuwa ajabu shabiki kwenda kumtunza mwanamuziki Sh. moja. Ilikuwa ni nyingi tu wakati huo. Ndiyo maana utaona kulikuwa mpaka na noti ya Sh. tano, kwa sababu haikuwa pesa ya mchezo.

Upande wa sarafu kulikuwapo; senti tano, senti kumi, senti hamsini 'sungura' ambayo ilijulikana zaidi kama thumni, Sh.moja hadi tano ya sarafu, Sh. tano ya sarafu iliyoitwa gwala au dala.

Hiyo ilisababisha hata beki mkuu namba tano kwenye mchezo wa mpira wa miguu akapewa jina la 'dala'. Hii ndiyo ilikuwa ndiyo thamani ya pesa ya Kitanzania kwa wakati huo. Ama kweli siku hazigandi!


BAJETI YA 1995/96

Kima cha chini kuwa Sh. 17,500

## Huduma ya Intaneti yarudishwa Sudan

**KHARTOOM,** SUDAN

SERIKALI ya mpito ya Sudan, imerejesha mtandao wa intaneti baada ya kusitisha huduma hiyo kwa muda wa mwezi mmoja baada ya jeshi kuondoa serikali ya kiraia.

Kampuni zote za mawasiliano zilirudishiwa huduma zao za mtandao juzi.

Kabla ya hatua hiyo, mahakama iliamuru kampuni tatu kubwa za mawasiliano nchini humo kurudishiwa huduma ya intaneti katika hukumu yake ya Novemba 9, lakini tatizo hilo liliendelea.

Kituo cha kuchunguza uhuru wa mtandao, Netblocks, pia kimethibitisha kurejeshwa kwa huduma hizo.

Kumekuwepo na maandamano ya kupinga mapinduzi katika mji mkuu Khartoum na maeneo mengine ya Sudan tangu Jenerali Abdel Fattah al-Burhan achukue mamlaka Oktoba 25 mwaka huu. Zaidi ya watu 30 wameripotiwa kuuawa katika maandamano hayo.

Hata hivyo, wanaharakati na makundi ya upinzani wamefaulu kusambaza picha za maandamano hayo kwenye mitandao ya kijamii licha ya kuwekewa vikwazo.

Akaunti rasmi ya Facebook ya Wizara ya Habari, ambayo inaambatana na Waziri Mkuu aliyeondolewa madarakani Abdalla Hamdok, pia imekuwa ikitumika kupaza sauti kupinga watawala wa kijeshi. **BBC**

## Wafanyakazi sita UN waachiwa huru

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

UMOJA wa Mataifa umthibitisha wafanyakazi wake sita wameachiliwa huru na serikali ya Ethiopia, na wengine watano bado wanaendelea kuzuiliwa.

Msemaji wa Umoja wa Mataifa Stephane Dujarric, alisema mtu mmoja wa familia na mfanyakazi wao pia wamezuiliwa.

Wafanyakazi hao wa UN, walikuwa miongoni mwa watu 16 waliozuiliwa mapema mwezi huu.

Hakuna sababu zilizotolewa za kuzuiliwa kwao na serikali ya Ethiopia haijasema chochote kuhusu kuachiliwa kwao.

Kumekuwa na visa vya watu kukamatwa nchini humo kufuatia kutangazwa kwa hali ya hatari.

Hata hivyo, majuzi serikali imekanusha kuwalenga watu maalum wakati wa kuwakamata, ikisema waliokamatwa wamekiuka sheria za dharura.

Mzozo kaskazini mwa nchi bado unaendelea huku vikosi vya serikali ya shirikisho vikipambana na waasi.

Kumekuwa na wito wa kimataifa kwa serikali na waasi kukomesha mzozo huo ambao umezidisha mzozo wa kibinadamu katika eneo hilo.

**BBC**

# Mfungwa anusurika kifo akiandaliwa kunyongwa

**OKLAHOMA,** MAREKANI

GAVANA wa Oklahoma nchini Marekani, amesitisha adhabu ya kunyongwa kwa mfungwa Julius Jones, saa chache kabla ya kutekelezwa kwake.

Kevin Stitt, alisema alikuwa akibadilisha kifungo hicho hadi kifungo cha maisha bila msamaha.

Kabla ya kutekelezwa kwa adhabu hiyo, mamia ya wanafunzi walitoka shuleni na kwenda ofisi ya gavana huyo wakidai Jones ahurumiwe.

Jones alihukumiwa kifo mwaka 2002, baada ya kupatikana na hatia ya kumuua Paul Howell, wakati wa utekaji nyara wa gari miaka mitatu iliyopita. Hata hivyo mshitakiwa huyo anasisitiza kwamba hana hatia

Kesi yake imevutia uungwaji mkono kutoka kwa watu mashuhuri akiwemo nyota wa televisheni ya Kim Kardashian na wanaharakati wa kupinga hukumu ya kifo.

Kunyongwa kwa Jones kwa kudungwa sindano ya kuua kuliratibiwa kufanyika saa 16:00 za huko (2200 GMT) katika gereza la serikali huko McAlester.

Lakini Govana Stitt, wa Republican, alisema aliingilia kati baada ya kuzingatia maombi na kukagua nyenzo zilizowasilishwa na pande zote za kesi hiyo.

Baraza la Msamaha la serikali hapo awali lilipendekeza katika kura ya wengi 3-1 kwamba hukumu ya Jones, ibadilishwe na kuwa kifungo cha maisha jela na uwepo uwezekano wa kuachiliwa huru.

Kesi hiyo imevutia kwa kiasi kikubwa atika miaka ya hivi karibuni, kwa sababu ya makala ya televisheni ya 2018 ya ABC "The Last Defense".

Zaidi ya watu milioni sita wametia saini ombi la kupewa haki kwa Julius, ambalo linasema alihukumiwa kifo kwa sababu ya migogoro ya kimsingi katika mfumo uliopewa jukumu la kuamua.

Jones alipatikana na hatia ya kumpiga risasi Howell, ofisa mtendaji wa bima, wakati wa wizi wa gari mnamo 1999 kwenye barabara ya kuingia kwake.


Mnamo Oktoba, alikuwa miongoni mwa watu watano walioshinda kesi za kuzuia kunyongwa kutoka kwa jopo la majaji watatu wa Mahakama ya Rufaa.

"Sikumuua Bw Howell," aliandika katika barua kwa bodi ya msamaha mwezi Aprili, baada ya kumaliza rufaa yake.

"Sikushiriki kwa vyovyote vile katika mauaji yake na mara ya kwanza nilipomuona kwenye televisheni wakati kifo chake kiliripotiwa." alijitetea

Lakini jamaa wa Howell walisema wito wa Jones wa kuomba msamaha umewakandamiza zaidi.

**BBC**



Julius Jones amenusurika kifo baada ya adhabu ya kunyongwa kutenguliwa saa chache kabla ya kutekelezwa **PICHA: MTANDAO**

## Imam auawa akituhumiwa kusaidia ugaidi

**KAMPALA,** UGANDA

KIKOSI cha usalama nchini Uganda kimemuua kwa kumpiga risasi mhubiri wa Kiislamu anayetuhumiwa kufanya kazi na kundi la watu wenye silaha wanaohusishwa na milipuko ya kujitoa mhanga katika mji mkuu Kampala.

Maofisa hao walisema Sheikh Muhammad Abas Kirevu, alikuwa amewaandikisha vijana kujiunga na shule za kigaidi zinazoendeshwa na Allied Democratic Forces (ADF), waasi ambao ni tiifu kwa kundi la Islamic State.Mauaji hayo yalifanyika nje kidogo ya Kampala.

Katika tukio hilo watu wanne waliuawa na washambuliaji waliokuwa kwenye pikipiki waliojilipua mjini humo siku ya Jumanne na wengine 30 walijeruhiwa katika shambulio hilo, ambalo IS ilithibitisha kuhusika kwake.

Kundi la wapiganaji wa Kiislamu la ADF, liliundwa nchini Uganda katika miaka ya 1990, lakini sasa lina makao yake katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Tangu lijiunge na IS mwaka 2019, limezidi kufanya mashambulizi kwa jina hilo.

Watu 21 wamekamatwa tangu shambulizi hilo litokee, huku polisi wakitaja kuwa ni harakati ya kuvunjwa kwa mtandao wa magaidi wa ADF nchini humo.

Msemaji wa polisi, Fred Enanga, alisema washukiwa 13 wakiwemo watoto kadhaa walinaswa walipokuwa wakijaribu kuvuka mpaka na kuingia DR Congo.

Siku ya Jumatano, washukiwa wanne wa ADF waliuawa karibu na mpaka huo.

Aidha, kikosi hicho kinaendelea kumtafuta imamu mwingine, Sheikh Suleiman Nsubuga, ambaye anatuhumiwa kutoa mafunzo, elimu ya itikadi kali na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya kutengenezea vilipuzi. **BBC.**

## Marekani yaiondolea vikwazo Burundi

**Washington** MAREKANI

Marekani imeondoa vikwazo vilivyowekwa dhidi ya Burundi vilivyodumu kwa miaka sita baada ya kuwepo mageuzi nchini humo.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, ilibainisha kuwa Rais Joe Biden, alibatilisha amri iliyoidhinisha vikwazo hivyo.

Marekani ilikubali uchaguzi wa mwaka jana ambao ulimuingiza madarakani Rais Évariste Ndayishimiye, ambaye anaendelea kufanya mageuzi katika sekta nyingi.

"Tunatambua hatua zilizoafikiwa na Rais Ndayishimiye, katika kushughulikia biashara haramu ya binadamu, mageuzi ya kiuchumi, na kupambana na rushwa na kuhimiza maendeleo endelevu," Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alisema.

Naibu Katibu wa Hazina ya Marekani, Wally Adeyemo, alisema katika taarifa tofauti kwamba Marekani itaendelea kuishinikiza Burundi kuboresha hali ya haki za binadamu nchini humo na kuwawajibisha wale wanaohusika na ukiukaji na unyanyasaji.


Marekani na Umoja wa Mataifa ziliweka vikwazo dhidi ya Burundi mwaka 2015, ikiwa ni pamoja na vikwazo vya visa na kufungia mali za maafisa wakuu serikalini.

Hatua hiyo, ilikuja baada ya nchi hiyo kuingia katika machafuko baada ya Rais Pierre Nkurunziza kuzindua azma ya kuwania muhula wa tatu madarakani.

Zaidi ya watu 1,000 waliuawa na mamia ya maelfu wengine walikimbia nchi katika ghasia zilizofuata. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DANIEL ANDREW UKWAYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S/128** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MALANGALI SEKONDARI mwaka 1980. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya Polisi: **DAR/CHU/RB/539452/2021.**

1165678402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI.**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA.**

**Usimamizi wa mirathi Na 58 /2021.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU VALERIA A. MUSHI wa DODOMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARY A. LEMASANI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 mwezi 11 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. **Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 11 mwaka 2021.

16 Mwezi 11 Mwaka 2021

**HAKIMU**

116578902

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Ndugu SILAJI ABEIDI WAKILI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki aina ya **Boxer - Bajaj** yenye namba za usajili **MC 394BJS,** injini namba **DUZWGC06846** na chessis namba **MD2A18AZ7GWC55018.** Ametoa taarifa polisi na kupewa RB namba **KAG/BUK/RB/548346/2021.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichoko karibu naye, au apige simu namba **0762250423.**

116578702

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **MUNZIRU MUSTAPHA ATHUMANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Hiace lenye namba za usajili **T123DSG,** injini namba **2RZ2292350** na chessis namba **RZH1254002799.** Ametoa taarifa polisi na kupewa RB namba **KAG/BUK/RB/534037/2021.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye au awasiliane na mhusika kwa namba **0753131422.**

116578802

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CARLYLE JOSEPH BOSSER** amepoteza kadi ya gari namba **T596AMS** aina ya Toyota Cresta Saloon. Taarifa ya kupotea imefunguliwa katika kituo cha Polisi Bukoba kwa kumbukumbu namba **KAG/BUK/RB/502482/2021.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

116578602

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP JUDICIAL CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 49 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late MARY TUMBO MAKMI**

**and**

**In the Matter of Application for letters of administration by PRISCA PROTUS TUMBO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 10th day of December, 2021.
Dated at DAR ES SALAAM this 19th day of November, 2021.

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo ...........PONGWE WILAYA TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi................48............2021**

**Ombi la... ANGEL DENNIS CURTIS ........Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu ....MOHAMMED NICO LEPTOS....**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 29/11/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 12/11/2021

Sahihi ya Hakimu

116580502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FORM II**

**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo PONGWE WILAYA TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 45/2021**

**Ombi la ROSE DANIEL FRANCIS Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu MARRY PATRICK JACOB**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 19/11/2021 kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kutenguliwa. Tarehe: 16/11/2021.

Sahihi ya Hakimu

116580502

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**probate and administration cause no.179 of 2021**

**In the matter of the estate of the late LEONARD JOSEPH BOYI of Chidachi West within Dodoma City**

**AND**

**In the matter of the application for letters of administration by JOYCE LEONARD BOYI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **20 day of NOVEMBER 2021.**
**Dated at Dodoma this 12 day of NOVEMBER 2021**

RESIDENT MAGISTRATE

116580702

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SUZANA MUHERE MURUNDI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 359 DDW.** Chassis namba **KGC120000126480.** Engine namba **IKR2854541.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/RB/5622/2021.**

115579802

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao walikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani nampenda kwa dhati. Alayempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-1

**Na Adam Fungamwangwo**
**(0716 350534)**

"Unaitwa nani binti?"

"Diana."

"Okay, una nafasi tukutane kesho Ilala kwenye hoteli ya Salmin?"

"Hapana kwa kesho sina nafasi labda wiki ijayo."

"Basi chukua 'biznesikadi' yangu huu, na wewe naomba namba yako."

Baada ya kupewa, jama kajitambulisha.

"Naitwa Dickson Chala, ni mmiliki wa kampuni yaa kusambaza mbolea mikoani."

"Ahsante nashukuru kwa kukufahamu. Alijibu Diana kwa sauti ya chini ya ya aibu."

Alikuwa amepewa lifti. Alikuwa anatoka zake kazini mitaa ya Posta, akielekea nyumbani kwao Kimara.

Kabla hajafika kituoni, gari aina ya Land Cruiser lilisimama mbele yake. Hakudhani kama lilisimama kwa ajili yake. Alipotaka kulipita aliona kioo kikishuka. "Mrembo panda nikusogeze" Alisikia sauti.

"Hapana, mi nimeshafika, naenda hapo tu." Aliongopa.

"Sawa hata kama umefika, kuna ubaya gani ukipanda, halafi nikakushusha hapo mbele?" Jamaa aling'ang'ania.

Ni maneno ambayo Diana aliona ni ya usumbufu. Kwa umri wa miaka 25 aliyonayo sasa ameshaona mengi. Ameshakutana na wanaume wa aina tofauti. Wenye mbinu tofauti za kutongoza wanawake.

Kuna wanaume ambao wao kumpata mwanamke ni lazima kwanza ajisifie hata kwa vitu vya uongo, ili mradi tu amehawishi akubali. Wakati mwingine anashia kucheza tu. Kwa sababu kuna mtu ambaye anajisifia, lakini kiuhalisia akimwangalia, hafanani na anavyovisema.

Ameshakutana na wanaume ambao kazi yao ni kutoa ahadi tu kubwa kubwa kwa wanawake, ili mradi tu atimize haja zao. Wapo wenye lugha tamu pia.

Lakini anachojua kati ya wote hao hakuna hata mmoja anayeweza kumlazimisha kufanya anatotaka kukifanya bila ridhaa yake.

Na hiyo ndiyo iliypomfanya aamue kupanda gari la mtu huyo ambaye alionekana ni mtu mwenye wadhifa, mwenye pesa, au yuko vizuri kiuchumi.




**Kifupi ni kwamba Diana alijua thamani ya uzuri wake tangu akiwa kinda. Alipotimiza miaka 15 tu, tayari wanaume wenye tamaa walianza kummezea mate.**

"Kumbe ulikuwa unanidanganya." Alisema Chala huku akijichekesha.

"Kukudanganya kivipi?"

"Si ulisema unakwenda mbele hapo? Hata mimi nilijua huendi mbele."

"Ni kweli, haiwezekani tu mimi nikubali tu kila lifti ninayopewa. Utakubali lifti za watu wangapi?" Alijibu Diana.

"Na kweli." Chala alijibu kabla ya kuulizwa swali "Unaelekea wapi nikupeleke mrembo?"

"Ubungo." Diana alidanganya tena. Hakutaka kumwambia Chala sehemu halisi anayoishi. Hakutaka usumbufu. "Kuna wanaume ukiwaonyesha sehemu unayoishi inakuwa ni matatizo tu. Mara tu kafika. Hupumui wala huna raha. Akikukuta hata na mwanaume tu ambaye mnafahamiana, tayari ugomvi." Aliwaza wakati akidanganya kuwa anaishi Ubungo. Kifupi ni kwamba Diana alijua thamani ya uzuri wake tangu akiwa kinda. Alipotimiza miaka 15 tu, tayari wanaume wenye tamaa walianza kummezea mate.

Labda uzuri wake ulitokana na mchanganyiko wa damu ya kibantu na kihindi. Mama yake alikuwa mfanyakazi wa ndani kwa mzee mmoja wa kihindi mjini Mbeya.

Wakati mama wa kihindi hayupo, mzee Khan alikuwa akichombeza hapa na pale kwa mama yake Diana.

Awali alikataa, lakini vizawadi vya hapa na pale na kuhakikishiwa maisha bora. Bishada aliona akikubali kutembea na mzee Khan basi maisha ya mnyanyaso yatakuwa yameisha mle ndani. Akakubali.

Na kweli ikawa hivyo. Mshahara wake ukaongezwa na akawa hacheleweshewi. Biashada akawa kama malkia mdogo kwenye nyumba ya mzee Khan, licha ya kwamba alikuwa akiingia asubuhi na kuondoka nyumbani jioni.

Wale wahenga waliosema penzi halina siri wala hawakukosea. Kuna waliosema penzi halisikiki, ila linaonekana. Mama wa kihindi akaanza kuhisi kuwa kuna mchezo ambao hauelewi unachezwa baina ya mumewe na binti wa kazi.

Alichofanya, akachachamaa hadi binti akatimuliwa kazi. Kwa bahati mbaya tayari alikuwa mjamzito. Mzee Khan alikuwa ameshaonja asali, akataka kuchonga mzinga. Alimpangia chumba sehemu. Akawa anakwenda kwa kujiiba kwa Bishada. Mtoto wa watu kitumbo nde.

Ujauzito haukuwa tatizo sana kwa mzee Khan na Bishada. Waliambiana tu iwe siri, Bishada asimtaje baba wa mtoto, ila atamhudumia hadi ajifungue na mtoto atatunzwa kama kawaida.

Ng'ombe wa masikini hazai. Mwezi mmoja tu kabla ya kujifungua, mzee Khan alipata ajali mbaya ya gari, ikawa mwisho wa Bishada kutesa. Tukio hilo lilimuumiza mno Bishada. Ikawa ndiyo mwanzo wa mateso. Alijifungulia mtoto kwa tabu. Matunzo yake pia alikuwa ya mashaka mashaka. Hata hivyo kila mmoja alijua kuwa mtoto wa kike ambaye Bishada alijifungua atakuwa msichana mrembo kutokana na rangi ya ngozi yake na sura yake pia. Na kila alipozidi kukua, ndipo uzuri ulipojitokeza dhahiri. Mtoto huyo alipewa jina la Diana. Hadi leo hii hakuna ndugu yoyote wa Bishada aliyejua baba ya mtoto huyo, ingawa tu waliambia ni mzee mmoja mwenye asili ya kihindi na ameshafariki dunia.

Umbile la Diana alilichukua kwa mama yake. Ni la kibantu, alikuwa na shepu halisi ya kiafrika. Umbo namba nane. Sura yake kwa mbali ilienda upande wa pili. Ilikuwa ni ya kiasia. Nywele nyingi hadi mgongoni, zilionekana kuwa amechukua kutoka upande wa baba. Ngozi nyeupe, pua iliyochongoka, vilimfanya Diana awe tofauti na warembo wengine.

Anapopita popote pale kila mmoja ni lazima amtazame mara mbilimbili. Labda kwa mtu ambaye hajamuona. Uzuri wale haukuwashangaza wanaume tu. Hata wanawake wenzake. Walishangaa kuona msichana na kibantu mwenye nywele ndefu kiasi kile, weupe, sura na pua kama ya kihindi.

Alikuwa kivutio vya wote. Na mwenyewe alilijua hilo. Ndiyo maana hakutaka kujiingiza kwenye mapenzi kirahisi kwa sababu alijua yeye ni kama ua. Kila nyuki analifuata. Lakini hakujua nyuki mwenye mapenzi halisi naye ni yupi. Hilo ndilo lilimtatiza.

"Hapa panatosha." Ilikuwa ni sauti yake, baada ya dakika mbili za ukimya.

"Okay mrembo, basi tutawasiliana, usisahau ahadi yetu."

"Hapana sisahau, ila ahsante sana."

"Usijali mrembo." Alisema Chala huku akiondoa gari taratibu, akizidi kuufaidi kwa macho uzuri wa Diana.

Chala alipagawa na msichana yule. Katika maisha yake alikuwa hajawahi kukutana na msichana ambaye amemfanya kusisimka na kushindwa hata maneno ya kuongea mbele yake kama yule.

ITAENDELEA JUMAMOSI

# UTAFITI UNYANYASAJI SOKA LA WANAWAKE WATOLEWA

**Na Saada Akida**

MKURUGENZI Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Michezo Nchini, Alex Nkeyenge, amesema ili kukuza zaidi soka la wanawake inatakiwa jamii kuhakikisha inaondoa fikra potofu kwa watoto wakike kwa ajili ya kushiriki kikamilifu katika mchezo huo.

Kauli mbiu katika mdahalo huo uliofanyika kwenye Ukumbi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ilikuwa ni "Ukatili wa Kijinsia Michezoni Haukubaliki".

Akizungunza katika uzinduzi wa mdahalo wa kitaifa uliohusisha utafiti kuhusiana na ukatili wa kijinsia katika soka la wanawake Tanzania, Nkeyenge ambaye alimwakilisha Naibu Waziri wa Wizara Sanaa, Utamaduni na Michezo, Pauline Gekul, alisema siku zote wanawake wakipewa fursa katika michezo huwa wanafanya vizuri na kuiletea nchi makombe mbalimbali.

Kiongozi huyo alisema jamii inatakiwa kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya wachezaji wanawake ili kuondoa fikira mbaya kwa wazazi.

Alisema anaamini baada ya mdahalo huo, jamii itapata mtazamo mwingine tofauti kuhusiana na soka la wanawake na itasaidia kuongeza mafanikio.

"Wanawake siku zote wakipewa fursa wanaweza, unaona jinsi tulivyowapa fursa katika michezo na wametuletea makombe, sasa inabidi tubadilike na kuwapa fursa wanawake kwa kushiriki mchezo wa mpira wa miguu kwani ni fursa na inajenga umoja, naamini italeta utofauti," alisema ofisa huyo.

Aliongeza anaamini matokeo ya utafiti huo yataongeza idadi ya wanawake katika ngazi ya uongozi lakini pia kutoa fikra potofu iliyokuwapo kwa muda mrefu katika mpira wa miguu kwa wanawake.

Naye Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Abdul-Latif Yassin, alisema katika mpira wa miguu wa wanawake wamekuwa na mwonekano tofauti hivyo wanatakia kutoka katika nadharia na kuingia kwenye uhalisia.

"Wachezaji wengi wa kike wamejiondoa katika uhalisia wao na kujiweka katika uhalisia wa kiume, hali ambayo viongozi wa timu au shirikisho husika wanatakiwa kukemea na kutolea adhabu," alisema Yassin.

Mkurugenzi wa Habari na Masoko wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Boniface Wambura, alisema kwa niaba ya Rais wa shirikisho hilo, Wallace Karia, soka la wanawake nchini limekuwa kwa kiasi kikubwa limefanikiwa kuipa nchi makombe manne kati ya 10 ndani ya kipindi cha miaka minne ya kiongozi huyo.

Wambura alisema TFF itaendelea kuhakikisha wanakuwa bega kwa bega na wachezaji wanawake ili kutokomeza unyanyasaiji wa kijinsia ambao unawazunguka.

"Eneo ambalo tumewekea mkazo zaidi ni kuhakikisha tunajenga soka la wanawake, kwani tunataka kutangaza mpira wetu zaidi kupitia soka la wanawake," alisema Wambura.

Katibu Mkuu wa Chama cha Soka cha Wanawake Nchini (TWFA), Somoe Ng'itu, alisema kupitia soka la wanawake wamepatikana viongozi, waamuzi na makocha ambao wanasimamia mpira hapa nchini.

"Sisi kwa pamoja tunaungana kupinga unyanyasaji wa kijinsia kwani wanawake wengi wapewa fursa na wamezitumia vyema, naamini kupitia utafiti huu kutakuwa na mabadiliko kwa jamii hasa kulikubali soka la wanawake," alisema Somoe.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Global Peace Foundation, Martha Ngambi, alisema kupitia utafiti huo amefurahi kubaini sababu mbalimbali zinazochangia unyayasaji wa kijinsia kwa wachezaji wanawake.

Nghambi alisema anaamini kupitia utafiti huo, matokeo chanya yatapatikana na wadau wanaohusika watahakikisha wanatokomeza ukatili huo.

Mtafiti kutoka Katika Chuo kikuu Dar es Salaam, Dk. Luciaus Mugisha alisema ili kuondoa ukatili huo anazitaka taasisi husika zinazosimamia mchezo huo kuweka miongozo iliyokuwa bora ambayo itamaliza na kutokomeza unyanyasaji.

# Stewate ashinda Jackpot bonus

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Bukoba, Juhudi Stewate (21), ameibuka mshindi wa Jackpot Bonus baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 na kujishindia kiasi cha Sh. milioni 11.

Akizungumzia ushindi wake, Juhudi alisema anafuraha sana kwa kuibuka mshindi na fedha aliyopata itamsaidia kwenye mambo yake mbalimbali.

"Nilianza kucheza na SportPesa tangu mwaka 2018, hivyo ni miaka mitatu sasa na niliifahamu hii kampuni kupitia rafiki yangu wa karibu. Nilikuwa nikiona akiweka 500/- na kushinda hadi elfu 40 nikashawishika sana na kuamua kuanza kucheza."

"Ukiachilia ushindi huu mkubwa tangu nianze kucheza nimewahi kushinda pesa kupitia ubashiri wa mechi moja moja lakini pesa kubwa niliyowahi kushinda ni Sh. 7700 tu."

"Mipango niliyonayo na pesa hizi ni mikubwa ikiwemo kununua viwanja nyumbani ili niweze kuwekeza, kufungua biashara ya nguo ambayo itaniendeshea maisha yangu ya kila siku na kuniingizia kipato na la mwisho kabisa ni kufunga ndoa."




Mshindi wa Sportpesa Jackpot Bonus Juhudi Stewart (21) kutoka Bukoba akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 11 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot ya wiki hii inayoshindaniwa ni Sh. milioni 686.9. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Akizungumza upande wa SportPesa, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti, Tarimba Abbas, alisema hii ni vizuri sana kuona tunaweza kubadili maisha ya vijana wadogo na kuinua kipato chao.

Tarimba alisema Sportpesa imeendelea kuwazawadia wateja wao zawadi mbalimbali na ndio maana hata kwa wanaobashiri Jackpot na wakapatia kwa usahihi kuanzia mechi 10 basi watabata bonus za viwango mbalimbali kulingana na ubashiri wao.

# Taifa Queens yalia na uzoefu

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Netiboli Tanzania (CHANETA), kimesema matokeo mabaya ambayo Timu ya Taifa ya mchezo huo (Taifa Queens), imeyapata katika mashindano ya Afrika imetokana na wachezaji wake kukosa uzoefu wa michezo ya kimataifa, imefahamika.

Taifa Queens imerejea nchini juzi kutoka Namibia ikiwa 'kichwa chini' baada ya kuondolewa katika hatua ya awali katika mashindano hayo ya Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa CHANETA, Devota Marwa, alisema kutokuwa uzoefu wa michezo ya kimataifa ilikuwa ni sababu mojawapo ya Taifa Queens kuyaaga mashindano hayo kwa kushindwa kukabiliana na ushindani uliokuwapo.

Marwa alisema Tanzania imekaa nje ya mashindano ya kimataifa kwa miaka saba muda ambao umeshusha kiwango cha wachezaji wa timu hiyo.

"Kutoshiriki mashindano ya kimataifa zaidi ya miaka saba ni sababu kubwa ya kutofanya vizuri katika michuano hii ya mwaka huu, tunasikitika tumeshindwa kupeperusha vyema bendera ya Taifa, haikuwa matarajio yetu," alisema Marwa.

Aliongeza njia pekee ya wachezaji kufanya vizuri ni kukiandaa kikosi kwa muda mrefu lakini pia kupata michezo mbalimbali ya kirafiki ya kimataifa ambayo italenga kuwajenga na kuwapa wachezaji uzoefu.

"Tukipata mechi nyingi za kimataifa ni imani yangu Tanzania tutarudi katika ubora wetu wa miaka ya nyuma, tutakuwa timu tishio katika mataifa mengine kwa siku za mbele,".

"Ushiriki wetu katika mashindano haya umetusaidia kurudi katika rekodi ya dunia ingawa bado hatujajua tuko katika nafasi ya ngapi, lakini muda si mrefu tutafahamu tuko katika nafasi ipi kwa Afrika," aliongeza bosi huyo.

Alisema mwaka huu walipata changamoto nyingine ya kuyaona mashindano hayo ni mapya kwa sababu ya baadhi ya sheria kubadilika huku maumbo makubwa ya wapinzani wao yalichangia kukiangusha kikosi chake.

## ZISIKUPITE

### PICKFORD AWANIWA
ANTONIO Conte anafikiria kumsajili golikipa, Jordan Pickford pale Tottenham Hotspur wakati wa dirisha dogo la Januari.**(Sky Sport)**

### ZIYECH KUTOLEWA
CHELSEA bado haijafanya uamuzi kuhusu majaliwa ya Hakim Ziyech, lakini kuna uwezekano akatolewa kwa mkopo Januari. **(Mail)**

### OLE KUWATUMIA NYOTA
OLE Gunnar Solskjaer anaweza kuwatumia Jesse Lingard, Donny van de Beek na Jadon Sancho kwenye mchezo dhidi ya Watford leo Jumamosi.

### LAMPARD ALIHOJIWA
FRANK Lampard alihojiwa kwa ajili ya kazi ya kuwa kocha wa Aston Villa lakini mchezaji mwenzake wa zamani wa timu ya taifa ya England, Steven Gerrard, ambaye alitajwa kuwa mrithi wa Dean Smith wiki iliyopita, mara zote alikuwa chaguo kubwa. **(Sun)**

### BRAYBROOKE KUSAINI
NAHODHA wa timu ya taifa ya England chini ya umri wa miaka 18, Sammy Braybrooke, atasaini mkataba na Leicester City licha ya Ujerumani kutaka kumnunua kiungo huyo mwenye umri wa miaka 17. **(Athletic, via Leicester Mercury)**

### NEUER AANZA MAZUNGUMZO
GOLIKIPA wa Ujerumani, Manuel Neuer, ameanza mazungumzo kuhusu kuongeza mkataba wake na Bayern Munich na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 anataka mkataba wa hadi angalau mwaka 2025. **(Sport1).**

### BALE NJE
MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 32, atakuwa nje ya uwanja kwa wiki tatu kutokana na jeraha la mguu baada ya kujiunga na Wales wakati wa mapumziko ya kimataifa. **(Marca)**

### LAPOTRA NA MESSI
RAIS wa Barca, Joan Laporta "hataondoa" uwezekano wa mshambuliaji wa Paris St-Germain Lionel Messi, 34, na kiungo wa kati wa Vissel Kobe Andres Iniesta, 37, kufuatia mchezaji mwenzao wa zamani Dani Alves kurejea katika klabu hiyo. **(Marca)**


### SWIFT AGOMBEWA
LEEDS United, Wolves na Burnley wanamnyatia kiungo wa Reading na mchezaji wa zamani wa timu ya taifa ya England chini ya miaka 21, John Swift mweye umri wa miaka 26. **(Sheffield Star)**

### CHO AWINDWA
AC Milan imeungana na Chelsea na Atletico Madrid katika mbio za kumuwania mshambuliaji wa timu ya taifa ya Ufaransa chini ya miaka 17, Mohamed-Ali Cho, kutoka Angers. **(L'Equipe)**

### LACAZETTE KUONDOKA
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 30, na mshambuliaji wa zamani wa timu ya taifa ya England chini ya miaka 21, Eddie Nketiah mwenye miaka 22, wanajiandaa kutimka Arsenal mikataba yao itakapomalizika katika majira ya joto. (Football London)

### JESSE MAMBO SAFI
NEWCASTLE United wanamatumaini kwamba fursa ya kuanza kikosi cha kwanza kutaongea nafasi yao ya kumsajili kiungo wa England Jesse Lingard mwenye miaka 28, kutoka Manchester United Januari. **(Northern Echo)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AIPA PANCHA PSG

## Ataikosa Nantes na City katika Ligi ya Mabingwa Ulaya kutokana...

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR ameondolewa kwenye kikosi cha Paris Saint-Germain kitakachoshuka dimbani leo Jumamosi dhidi ya Nantes na pia yupo shakani kuivaa Manchester City ugenini kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya, kwa mujibu wa L'Equipe.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 alikosa mchezo wa kufuzu kombe la Dunia wa Brazil dhidi ya Argentina Jumanne iliyopita kutokana na kuwa majeruhi, ambayo aliyapata kwenye ushindi wa 1-0 dhidi ya Colombia.

Gazeti la L'Equipe limeripoti kwamba, Neymar amefanyiwa vipimo baada ya kurudi Ufaransa na imeonesha wazi hataweza kucheza dhidi ya Nantes Jumamosi hii.

Majeruhi hayo pia yanamuweka kwenye wakati mgumu kucheza mchezo wa Jumatano wa Ligi ya mabingwa Ulaya wakundi A dhidi ya Man City.

Kikosi hicho cha kocha Pep Guardiola, City kinaongoza msimamo wa kundi kikiwa na pointi tisa, huku PSG ikiwa nafasi ya pili kwa pointi zake nane, nne zaidi ya Club Brugge iliyopo nafasi ya tatu.

Iliripotiwa kwamba, Marco Verratti na Presnel Kimpembe ambao walikuwa majeruhi wamerudi kwenye mazoezi na wana uwezekano mkubwa wa kurudi dimbani leo.

Nyota wa zamani wa Real Madrid, Sergio Ramos pia amerudi kwenye mazoezi na kuna uwezekano mkubwa ataanza mchezo wake wa kwanza dhidi ya Nantes leo.

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 686




# RODGERS AIKATAA OFA YA UNITED



**LONDON, England**

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, amekataa kuhusishwa na kazi ya Manchester United.

Iliripotiwa kwamba, Rodgers ndio mtu namba moja anayewania kazi ya Mashetani wekundu hao ili kuchukua mikoba ya Ole Gunnar Solskjaer ambaye amekalia kuti kavu.

Solskjaer amekuwa kwenye presha kubwa msimu huu, huku United wakiwa nafasi ya sita kwenye msimamo, wakichapwa mabao 5-0 nyumbani na Liverpool, pia wakipoteza 2-0 kutoka kwa Manchester City pale Old Trafford.

Na Rodgers Alhamisi alibainisha kwamba, yeye akili yake ni kuiongoza timu yake dhidi ya mabingwa wa kombe la FA Chelsea pale kwenye uwanja wa King Power leo Jumamosi.

Kocha huyo wa zamani wa Liverpool na Celtic aliwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo huo: "Kuna vitu viwili. Kwanza, si heshima kuuliza swali la kuchukua nafasi ya kocha mwingine, yeye ni kocha mzuri na mtu mzuri, na anafanya kazi nzuri kwenye klabu yake.

"Pili, siwezi kutoa kauli yoyote kuhusu hilo, kwa sababu sio kitu kizuri.

"Mimi ni kocha wa Leicester City, najisikia fahari kuwa hapa, na akili yangu ni kuhakikisha timu inafanya vizuri.

"Hivyo sikifirii nafasi nyingine, kwa sasa nipo hapa na nitaendelea kuwa hapa."

# Jesse: Nataka kuondoka Man United



**MANCHESTER, England**

JESSE Lingard amesisitiza kuwa anataka kuondoka baada ya mazungumzo na klabu ya Manchester United kuhusu mkataba mpya kushindikana.

Lingard alikataa mkataba alioandaliwa na Man United Oktoba, ambao ulikuwa na thamani ndogo kuliko aliokuwa nao sasa hivi.

Kwa sasa nyota huyo hana mpango wa kufungua milango kwa mazungumzo mengine na miamba hiyo ya Old Traford.

Lingard anatarajia kutolewa kwa mkopo baada ya kupata nafasi chache, tokea kuwasili kwa Cristiano Ronaldo hapo kwenye viunga vya Carrington Park licha kuonesha kiwango kikubwa alipotolewa kwa mkopo kwenda klabu ya West Ham.

Lingard baada ya mazungumzo ya mkataba mpya kushindikana anatarajia kuondoka kama mchezaji huru majira ya kiangazi mwakani.

Klabu kubwa za Ulaya nimeonesha nia ya kutaka saini yake zikiwamo Barcelona na AC Milan

# HABARI MICHEZO

6,934,380

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 20.11.21 | 18:00 | Burnley vs Crystal Palace | 2.80 | 3.21 | 2.55 |
| 2. 20.11.21 | 18:00 | Aston Villa vs Brighton | 2.50 | 3.25 | 2.85 |
| 3. 20.11.21 | 18:00 | Newcastle vs Brentford | 2.69 | 3.24 | 2.64 |
| 4.20.11.21 | 18:00 | Wolverhampton vs West Ham | 3.01 | 3.21 | 2.41 |
| 5. 20.11.21 | 18:00 | Hull City vs Birmingham | 2.63 | 3.12 | 2.63 |
| 6. 20.11.21 | 18:00 | Reading vs Nottingham | 2.89 | 3.18 | 2.39 |
| 7. 20.11.21 | 20:00 | Lazio vs Juventus | 2.78 | 3.36 | 2.48 |
| 8. 20.11.21 | 20:45 | Sparta Rotterdam vs Twente | 2.61 | 3.20 | 2.61 |
| 9. 20.11.21 | 22:45 | Fiorentina vs AC Milan | 3.09 | 3.39 | 2.26 |
| 10. 21.11.21 | 15:00 | Brest vs Lens | 3.03 | 3.43 | 2.26 |
| 11. 21.11.21 | 17:00 | Salernitana vs Sampdoria | 3.00 | 3.29 | 2.37 |
| 12. 21.11.21 | 17:00 | Troyes vs St Etienne | 2.35 | 3.34 | 2.94 |
| 13. 21.11.21 | 17:00 | Metz vs Bordeaux | 2.42 | 3.28 | 2.88 |

## MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 20 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3603 | Mbeya City vs Mtibwa Sugar | 1.74 | 3.45 | 5.20 |
| 14:05 | 3025 | Perth Glory vs Adelaide United | 2.27 | 3.39 | 2.95 |
| 15:30 | 1154 | Leicester vs Chelsea | 4.50 | 3.70 | 1.76 |
| 15:30 | 2551 | Sheffield Utd vs Coventry | 1.99 | 3.34 | 3.58 |
| 16:00 | 2792 | Namungo vs Young Africans | 6.40 | 3.45 | 1.63 |
| 16:00 | 2832 | Celta Vigo vs Villarreal | 2.80 | 3.30 | 2.50 |
| 16:00 | 5812 | Kagera Sugar vs Geita Gold FC | 1.79 | 3.20 | 5.40 |
| 17:00 | 3840 | Atalanta vs Spezia | 1.25 | 6.40 | 9.60 |
| 17:30 | 1968 | Arminia Bielefeld vs VfL Wolfsburg | 3.93 | 3.48 | 1.91 |
| 17:30 | 2095 | Monchengladbach vs Greuther Furth | 1.29 | 5.78 | 8.77 |
| 17:30 | 3189 | Borussia Dortmund vs Stuttgart | 1.33 | 5.37 | 7.76 |
| 17:30 | 3479 | Bayer Leverkusen vs VfL Bochum | 1.39 | 4.99 | 6.98 |
| 17:30 | 4474 | Hoffenheim vs RB Leipzig | 3.89 | 4.09 | 1.78 |
| 18:00 | 1342 | Hull City vs Birmingham | 2.55 | 3.09 | 2.75 |
| 18:00 | 1424 | Reading vs Nottingham | 2.94 | 3.19 | 2.34 |
| 18:00 | 1511 | Middlesbrough vs Millwall | 2.09 | 3.19 | 3.48 |
| 18:00 | 1804 | Fulham vs Barnsley | 1.24 | 5.73 | 9.87 |
| 18:00 | 1878 | Dundee Utd vs Aberdeen | 3.05 | 3.10 | 2.36 |
| 18:00 | 2560 | Stoke City vs Peterborough | 1.50 | 4.21 | 5.69 |
| 18:00 | 3679 | Bristol City vs Blackburn | 2.94 | 3.33 | 2.28 |
| 18:00 | 3710 | Watford vs Manchester Utd | 5.47 | 4.25 | 1.56 |
| 18:00 | 3971 | Preston vs Cardiff | 2.14 | 3.29 | 3.24 |
| 18:00 | 4644 | Burnley vs Crystal Palace | 2.78 | 3.18 | 2.59 |
| 18:00 | 4662 | Wolverhampton vs West Ham | 2.94 | 3.29 | 2.41 |
| 18:00 | 4884 | Huddersfield vs West Bromwich | 3.64 | 3.19 | 2.03 |
| 18:00 | 4921 | Newcastle vs Brentford | 2.64 | 3.29 | 2.64 |
| 18:00 | 5211 | Shakhtar Donetsk vs Rukh Vinnyky | 1.10 | 7.33 | 18.33 |
| 18:00 | 5274 | Swansea vs Blackpool | 1.85 | 3.44 | 4.03 |
| 18:00 | 5397 | Motherwell vs Hearts | 3.40 | 3.40 | 2.05 |
| 18:00 | 5402 | Raith Rovers vs Morton | 1.74 | 3.52 | 4.40 |
| 18:00 | 5506 | Aston Villa vs Brighton | 2.38 | 3.31 | 2.96 |
| 18:00 | 5991 | Norwich City vs Southampton | 3.50 | 3.40 | 2.08 |
| 18:15 | 5384 | Sevilla FC vs Alaves | 1.44 | 4.39 | 7.38 |
| 18:30 | 2275 | PSV Eindhoven vs Vitesse Arnhem | 1.39 | 4.81 | 6.48 |
| 19:00 | 1025 | FC Krasnodar vs Spartak Moscow | 1.88 | 3.65 | 3.65 |
| 19:00 | 1214 | Josko Ried vs TSV Hartberg | 2.55 | 3.23 | 2.51 |
| 19:00 | 3172 | RB Salzburg vs Admira Wacker | 1.05 | 9.28 | 23.20 |
| 19:00 | 4282 | Alanyaspor vs Besiktas | 2.71 | 3.40 | 2.43 |
| 19:00 | 5985 | Paris St Germain vs Nantes | 1.32 | 5.29 | 8.57 |
| 20:00 | 5008 | Lazio vs Juventus | 2.88 | 3.32 | 2.43 |
| 20:30 | 1186 | Union Berlin vs Hertha BSC | 1.96 | 3.37 | 3.87 |
| 20:30 | 3356 | Atletico Madrid vs Osasuna | 1.43 | 4.30 | 7.80 |
| 20:30 | 5047 | Liverpool vs Arsenal | 1.49 | 4.71 | 5.61 |
| 20:45 | 2381 | Sparta Rotterdam vs Twente | 2.65 | 3.14 | 2.60 |
| 21:00 | 3273 | Sporting Braga vs Santa Clara | 1.31 | 4.81 | 7.88 |
| 22:00 | 3863 | AZ Alkmaar vs NEC Nijmegen | 1.34 | 4.92 | 7.68 |
| 22:45 | 4865 | Fiorentina vs AC Milan | 3.21 | 3.46 | 2.18 |
| 23:00 | 4074 | Rennes vs Montpellier | 1.52 | 4.38 | 5.57 |
| 23:00 | 4786 | Barcelona vs Espanyol | 1.42 | 4.66 | 7.08 |
| 23:15 | 1332 | Porto vs CD Feirense | 1.10 | 7.50 | 18.27 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# XAVI KUANZA KAZI DHIDI YA ESPANYOL



**BARCELONA, Hispania**

MASHABIKI wa sehemu mbalimbali duniani kwa sasa wanasubiri kumuona Xavi akiwa kwenye benchi la Barcelona na kubeba mzigo uliowashinda wenzie kwenye viunga vya pale Camp Nuo.

Baada ya kufanya vizuri nchini Qatar na staili yake ya soka la tiktaki ambayo iliasisiwa na Johan Cryuf na kutumiwa vizuri kabisa na kocha Pep Gurdiola sasa mashabiki wanahamu ya kuona Xavi akiirudisha tena kwenye viunga vya Camp Nou.

Barcelona leo Jumamosi wanawakaribisha Espanyol kwenye dimba la Camp Nou huku baadhi ya wachezaji nao wakirejea kutoka kwenye michezo ya kimataifa na wale majeruhi Pedri and Osumane Dembélé wakitarajiwa kurudi kwenye mchezo wa ligi ya mabingwa dhidi ya Benfica.

Xavi tangu achukue mikoba ya kuinoa klabu hiyo amefanya mabadiliko makubwa huku akitumbua majipu ambayo alihisi ni kikwazo kwa mafanikio ya Barcelona.

Huo unakuwa mchezo wake wa kwanza Xavi kuinoa Barcelona dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja.

# Hazard hana furaha kwa sasa – Martinez



**BRUSSLES, Ubelgiji**

KOCHA wa timu ya taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez, amekiri kuwa Eden Hazard kwa sasa ni mtu asiye na furaha linapokuja suala la soka.

Hazard bado hajaweza kuyafikia matarajio ya wengi klabuni Real Madrid, tangu alipokamilisha uhamisho wa fedha nyingi kutoka Chelsea.

Changamoto ya majeraha imekuwa ikiathiri kiwango cha nyota huyo, na hata alipokuwa poa alishindwa kufanya vizuri kama ambavyo ilikuwa inatarajiwa kwake.

Licha ya msimu huu kuwa katika hali yake nzuri kiafya, bado hajaweza kumshawishi kocha Carlo Ancelotti kumpa kipaumbele kwenye kikosi chake cha kwanza.

Martinez aliamua kuzungumzia mtazamo wake juu ya hali ya Hazard kisoka kwa sasa, na akanukuliwa akisema;

"Tunahitaji afike Kombe la Dunia akiwa amejiandaa. Tumekuwa na kikosi kikubwa kwa sasa.

"Eden yupo katika kipindi cha mfadhaiko kwa upande wa soka," alisema Martinez.

Hazard kwa sasa anapambania kurejea kwenye ushawishi mkubwa kwa kocha Ancelotti.

# Michezo

Jumamosi Novemba 20, 2021

Nipashe




## Neymar aipa pancha PSG

UKURASA 21



Mshambuliaji wa Simba, Kibu Dennis (mwenye rasta), akifunga bao la tatu katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza jana. Simba ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YATEMA CHECHE

●●●Yaichapa Ruvu Shooting mabao 3-1 huku rekodi ya Manula...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu mpya wa Simba, Mhispania Pablo Franco, ameanza kibarua chake kwa kishindo baada ya kuichapa Ruvu Shooting mabao 3-1 katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza jana.

Ushindi huo unaifanya Simba ifikishe pointi 14, pointi moja pungufu dhidi ya vinara wa ligi hiyo, Yanga, ambao leo watashuka kuwakabili Namungo FC, katika mchezo mwingine wa ligi hiyo.

Yalikuwa ni mabao mawili ya Meddie Kagere yanayomfanya afikishe magoli manne kwenye orodha ya wafungaji na moja la Kibu Dennis ambalo ni la kwanza kwake tangu ajiunge na mabingwa hao watetezi msimu huu akitokea Mbeya City.

Hata hivyo kwenye mechi hiyo, rekodi ya golikipa, Aishi Manula, kutoruhusu mabao kwenye mechi tano, imevunjwa rasmi, baada ya kutunguliwa bao na straika wa zamani wa timu hiyo, Elius Maguri.

Ikumbukwe Ruvu Shooting, pia ilitibua rekodi ya kipa wa Yanga, raia wa Mali, Djigui Diarra ambaye alitunguliwa kwenye mechi ya raundi ya tano, baada ya kucheza mechi nne bila kuruhusu bao.

Hiki ni kipigo cha pili mfululizo kwa Ruvu Shooting ambayo ilifungwa idadi kama hiyo ya mabao Novemba 3, mwaka huu ilipokutana na Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ni mechi iliyoonekana timu hizo kugawana vipindi, Simba ikitawala kipindi cha kwanza huku Ruvu Shooting walitandaza kambumbu safu dakika 45 za kipindi cha pili. Kipa wa Ruvu Shooting, Mohamed Makaka, alifanya kazi ya ziada dakika ya tisa na 10 alipookoa michomo hatari iliyoonekana ingewapa Simba mabao ya mapema.

Kwanza ilikuwa ni faulo ya Bernard Morrison dakika ya tisa, ambayo ilionekana inatinga wavuni, lakini aliruka juu na kuipiga ngumi iliyozaa kona ambayo pia ilikwenda kuchongwa na Morrison, ikaunganishwa na Kibu kabla ya kipa huyo kwenda tena juu na kuupangua.

Simba ikionekana kushambulia mfululizo, ilipata bao la kwanza dakika ya 17 kupitia kwa Kagere, ukiwa ni mpira wa kona uliopigwa na Morrison ambao ulikoswa kuunganishwa na Paschal Wawa, ukamkuta Kagere aliyeudokoa na kutinga wavuni, licha ya juhudi kubwa za kipa Makaka kutaka kuuokoa.

Almanusura Simba iandike bao dakika ya 26, baada ya Hassan Dilunga kuukokota mpira na kutinga ndani ya eneo la hatari, akaachia shuti kali lililopaa juu la lango.

Kagere alifunga bao la pili baada ya kazi nzuri ya Kibu aliyeingia ndani ya eneo la hatari na kupiga shuti dhaifu, lakini lilitemwa na Makaka, mfungaji akaubetua kidogo huku dakika moja kabla ya mapumziko, Kibu alifunga bao lake la tatu kwa Simba.

Ilikuwa ni krosi ya Shomari Kapombe iliyomkuta Kagere ambaye aliupiga kwa kisigino, ukawapoteza maboya kipa Makaka na mabeki wake, na kumkuta mfungaji akiwa hana kazi kubwa, zaidi ya kuweka tu mguu, mpira ukakwama wavuni. Kipindi cha pili wenyeji waliingia kwa kasi na kuwapa wakati mgumu Simba, kiasi cha kulazimika kufanya mabadiliko ya kuwatoa Kagere, Morrison, Mzamiru Yassin, Mohamed Hussein na Hassan Dilunga na kuwaingiza Erasto Nyoni, Duncan Nyoni, Pape Sakho, Yusuph Mhilu, na Gadiel Michael.

Juhudi ya Ruvu Shooting kuishambulia Simba kwa muda mrefu, zilizaa matunda dakika ya 70, baada ya Maguri aliunganisha mpira uliopigwa ndani ya eneo la hatari, huku mabeki wa timu pinzani wakichelewa kuuondosha.

Dakika moja baadaye, Simba ilikosa penalti ya pili msimu huu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyopigwa na Erasto na kupanguliwa kwa ustadi na kipa Makaka. Penalti hiyo ilitokana na Kibu kuwatuliwa na Zuberi Dabi kwenye eneo la hatari.

## Yanga, Namungo muda wa hukumu

**Na Mwandishi Wetu**

MBIO za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara zinatarajia kuendelea tena leo kwa vinara, Yanga kutoka jijini Dar es Salaam wakiwashuka kuwavaa wenyeji Namungo FC katika mechi ya raundi ya sita itakayochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Yanga inaingia dimbani ikiwa na lengo moja tu la kuendeleza ushindi wake wa asilimia 100, baada ya kuvuna pointi 15 kwenye mechi zake tano ilizocheza.

Kikosi hicho cha Yanga kiliwasili Lindi juzi jioni tayari kwa mechi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na ushindani kutoka kwa timu zote mbili.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako tayari kuwakabili wapinzani wao na wamejiandaa kuendeleza kasi ya ushindi kwenye ligi hiyo.

Nabi alisema anafahamu mchezo huo utakuwa na ushindani kutokana na ubora wa viwango vya wachezaji wa Namungo.

Kocha huyo alisema kila mchezo kwake ni muhimu na wamejiandaa kuongeza umakini na utulivu kila watakapokuwa na mpira.

"Ninafahamu tutakutana na moja ya timu bora, ninawafahamu, ninajua ni aina gani ya soka wanalocheza," alisema Nabi.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliwataja wachezaji watakaokosa mechi hiyo kutokana na kuwa majeruhi ni Ramadhani Kabwili, Mapinduzi Balama, Dickson Ambundo na Yacouba Songne aliyefanyiwa operesheni.

"Wachezaji walioko wote wana uwezo na yoyote atakayepangwa na mwalimu, basi anaweza kuitumikia Yanga," alisema Bumbuli.

Naye Kocha Msaidizi wa Namungo, Godfrey Okoko alisema wamedhamiria kuzibakisha pointi tatu kwenye ardhi ya nyumbani

"Tumefanya maandalizi mazuri, na tuendelea kujiandaa. Wachezaji wako fiti, mambo yote mpaka sasa tuko sawa. Tutashinda hii mechi, mashabiki wa Namungo wasiwe na wasiwasi. Yanga ni timu kubwa na tunaiheshimu, Namungo ni timu kubwa pia. Mpaka sasa wachezaji wetu wanajua hawajafanya vizuri kwa hiyo wanataka kuwaonyesha mashabiki kwenye mechi hii ili warejeshe furaha," alisema kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042